# KANUNI ZA SHARIA ZA KIISLAMU

## (UTANGULIZI WA MFUMO WA ELIMU YA FIQHI)

**Kimeandikwa na:**
Mohammad Ali Shomali

ترجمة

# أصول الفقه

تأ ليف

محمد علي شومالى

من اللغة الإنجليزية  الى اللغة السواحلية

09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd   2    9/9/2015   12:56:00 PM

**©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**
**AL-ITRAH FOUNDATION**

**ISBN: 978 - 9987 – 17 – 025 – 8**

**Kimeandikwa na:**
Dr. Mohamed Ali Shomali

**Kimetarjumiwa na:**
Alhaji Ramadhani S. K. Shemahimbo

**Kimehaririwa na:**
Al Haji Hemedi Lubumba Selemani

**Kimepitiwa na:**
Sheikh Hassan Ali Mwalupa

**Kimepangwa katika Kompyuta na:**
Al-Itrah Foundation

**Toleo la kwanza:** Decemba, 2015
**Nakala:** 1000

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**
Alitrah Foundation
S.L.P. - 19701, Dar es Salaam, Tanzania
**Simu:** +255 22 2110640 / 2127555
**Barua Pepe:** alitrah@yahoo.com
**Tovuti:** www.ibn-tv-com
**Katika mtandao:** www.alitrah.info

# YALIYOMO

Neno La Mchapishaji........................................................................ 1

Utangulizi...................................................................................... 1

**SOMO LA KWANZA: MISINGI YA SHARIAH (FIQH) ..... 6**

Kanuni ........................................................................................ 6

Hukumu (Fat-wa)........................................................................ 7

Aina za Hukumu ........................................................................ 8

Chanzo ........................................................................................ 9

Maudhui ya Misingi ya Shariah .................................................... 10

Faida ya Misingi ya Shariah ........................................................ 10

**SOMO LA PILI: MGAWANYIKO WA HUKUMU ............. 11**

Upambanuzi wa Shuruti ............................................................. 11

**SOMO LA TATU: VYANZO VYA REJEA ............................ 17**

Qur'ani Tukufu ............................................................................ 17

Sunnah ........................................................................................ 19

Upambanuaji wa Hadithi ............................................................. 24

**SOMO LA NNE: MAANDISHI (MATINI) ............................ 29**

**SOMO LA TANO: MAAMRISHO NA MAKATAZO ......... 35**

Makatazo ........................................................................................ 38

**SOMO LA SITA: MAANA YA WAZI .................................... 41**

Maana ya Masharti ............................................................................ 43

Maana Inayoambatana na Sifa ........................................................ 45

Maana Iliyokusudiwa ........................................................................ 46

**SOMO LA SABA: JUMLA NA DHAHIRI ............................ 48**

Aina tofauti za Ujumla .................................................................... 49

Aina tofauti za Umaalum ................................................................. 50

Maalum na Kimasharti ..................................................................... 52

**SOMO LA NANE: KANUNI ZA KILUGHA......................... 54**

Uhusiano kati ya Qur'ani na Sunnah ........................................... 55

**SOMO LA TISA: MGONGANO BAINA YA RIWAYA ....... 58**

**SOMO LA KUMI:**
**MAKUBALIANO YA PAMOJA (IJMAH) .............................64**

Upambanuaji wa Makubaliano (Ijmah) ....................................... 64

Uhusiano kati Makubaliano na Sunnah ....................................... 65

**SOMO LA KUMI NA MOJA: AKILI .................................... 67**

1. Kutosha ........................................................................................ 70

2. Masharti juu ya Wajibu ............................................................ 72
3. Kinyume Chake ...................................................................... 75
4. Mkusanyiko wa Amri na Makatazo .......................................... 76
5. Kuingia kwa Batili Kutokana na Makatazo .............................. 78

**SOMO LA KUMI NA MBILI:**
**KANUNI ZA KIMATENDO ...................................................80**

Kanuni ya Muendelezo ................................................................ 81
Kanuni ya Kusamehewa ............................................................... 82
Kanuni ya Tahadhari .................................................................... 84
Kanuni ya Chaguo (Hiari) ............................................................ 85



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 6 9/9/2015 12:56:00 PM

# NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu ulichonacho mikononi mwako ni tarjuma ya Kiswahili ya kitabu cha Kiingereza kilichoandikwa na Mohammad Ali Shomali kiitwacho, *Principles of Jurisprudence*. Sisi tumekiita, Kanuni za Sharia za Kiislamu.

Uislamu ni dini na ni mfumo kamili wa maisha. Maana yake unahudumia roho na mwili. Kwa hiyo umeweka sheria na kanuni zenye kukidhi maisha ya hapa duniani na maisha ya kesho Akhera.

Katika kitabu hiki mwandishi ameainisha na kuelezea baadhi ya kanuni na sheria ambazo kwazo mwanadamu anatakiwa azizingatie ili apate kuishi maisha bora na kufuzu kiroho ili akaishi maisha bora ya milele kesho Akhera.

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana, husasan wakati huu wa maendeleo makubwa ya kielimu ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia ni vitu ambavyo havina nafasi katika akili za watu.

Kutokana na ukweli huu, taasisi yetu ya al-Itrah imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumini yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu, husussan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu al-Haj Ramadhani S. K. Shemahimbo kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kukitarjumi kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake. Allah awalipe wote malipo mema hapa duniani na kesho Akhera. Amin!

**Mchapishaji**
**Al-Itrah Foundation**

# UTANGULIZI

Suala muhimu sana kwa mwanafunzi wa dini mbalimbali ni kugundua ile njia ambayo mafundisho ya dini hiyo yanaweza kusomwa kwa utaratibu na inavyoweza kufasirika kwa namna ya kuridhisha kutoka kwenye vyanzo vyake. Hapa maswali mawili muhimu yanajitokeza: Kwanza, ni vyanzo gani vya dini hiyo ambavyo wafuasi wake wote wanavishikilia na ni juu ya uchunguzi gani wowote kuhusu dini hiyo utakaokuwa umetegemea? Pili, ni njia gani sahihi ya kuvielewa vyanzo hivyo?

Katika Uislam kuna njia mbili tofauti za vyanzo ambavyo juu yake uchunguzi juu ya Uislam lazima utegemezwe: Wahyi na akili (mantiki). Namna ya kujifunza wahyi ni kurejea kwenya Qur'ani na Sunnah. Namna ya kuelewa hukumu za kiakili ni kufuata kanuni za mantiki na kujenga hoja za kiakili zisizo na shaka. Katika vile vipengele vya dini ambavyo ndani yake hakuna fursa ya kutumia akili kwenye ukweli unaohusika, kama vile maelezo mengi ya ufufuo na hukumu za kimatendo za Shariah, mtu anaweza kuongozwa tu na ushahidi uliofunuliwa. Katika kuthibitisha ukweli wa dini au wa Nabii, ambamo kurejea kwenye ushahidi uliofunuliwa kunahusisha kuzungushana katika suala hilo na kusababisha mabishano ya mzunguko hapo mtu anaweza kutumia hoja huru za kimantiki, kama vile kuthibitisha kuwepo kwa Mwenyezi Mungu na ukweli wa mambo fulani ya kidini au Nabii. Mtu hawezi kuhojiana juu ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu au ukweli wa Uislam kwa kurejea tu kwenye aya fulani fulani za Qur'ani au kunukuu baadhi ya semi za Qur'ani.

Kuna masuala ambamo vilevile vyanzo vyote na njia zote zinaweza kufanya kazi, kama vile nyingi ya sifa za Mwenyezi Mungu au hesabu za haki za Mwenyezi Mungu au sifa za msingi za uadilifu



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 2 9/9/2015 12:56:01 PM

au uharamu wa vitendo vya dhulma kutoka kwenye mtazamo wa kifiqihi.

Elimu ya *Usuul al-Fiqh* ni udhibiti ambao unazichunguza njia za kuelewa vyanzo vya Kiislam, au kwa usahihi zaidi, njia za kuelewa mafunzo ya Kiislam kutoka kwenye vyanzo vyake. Ingawa mwanzoni ilianzishwa kuwasaidia mafaqihi wa Kiislam katika kuelezea njia zinazofaa za kufikia fatwa za hukumu za kisheria za Kiislam kutoka kwenye vyanzo vyake halali, *Usuul al-Fiqh* inaweza kwa hakika kuwa yenye msaada, na kwa kweli ya muhimu katika nyanja nyinginezo za mafunzo ya Kiislam pia. Kwa uchunguzi wowote kuhusu Uislam, ima kwenye itikadi, sheria au hata tabia njema (*akhlaq*) kunahitajia kurejea kwenye Qur'ani, Sunnah na akili.

Hii ndio sababu nina shaka kiasi fulani juu ya kuchukulia *Usuul al-Fiqh* kama "utaratibu wa fiqh ya Kiislam" tu. *Usuul al-Fiqh*, hususan baada ya maendeleo yaliyofanywa na Sheikh Murtadha Ansari na warithi wake, imekuwa ni elimu kubwa sana na ya kisasa ambayo inazungumzia masuala mengi ya kiutaratibu wa elimu nyingine za Kiislam, kama vile masomo ya Qur'ani na hadith, maadili na theiolojia. Bila shaka vile vipengele vya *Usuul al-Fiqh* vinavyoshughulika na elimu nyingenezo mbali na fiqihi bado vinahitaji kuendelezwa. Inatarajiwa kwamba elimu iliyopo sasa ya *Usuul al-Fiqh* itaendelezwa na kuwa sayansi ya mwamvuli mpana inayoweza kushughulika na mas'ala ya jumla ya utaratibu wa masomo ya Kiislam yenye matawi fulani yenye taratibu maalum za kila elimu. Vilevile kuna matatizo ya kifalsafa, kitheolojia na kimaadili ambayo kwa sasa yanachunguzwa katika *Usuul al-Fiqh*, lakini yanaweza yakaachwa kwenye udhibiti wao husika, kama vile suala la hiari na wema na uovu wa asili.

Kitabu hiki cha sasa ni jaribio dogo jepesi tu la kuitambulisha hii sayansi iliyozama kwa wasomaji wa lugha ya Kiingereza. Bila

shaka pamekuwa na majaribio yaliyopita kuhusiana na hili, kama vile tafsiri mbili za *Al-Halqah al-Uulaa* cha Ayatullah Sayyid Muhammad Baqir al-Sadr kwa Kiingereza: kingine cha Arif Husein kiitwacho *Principles of Islamic Jurisprudence According to Shi'i Law*, na kingine pia cha Roy Muttahidah kama *Lessons in Islamic Jurisprudence*. Hata hivyo, bado kuna mwanya mkubwa katika kuitambulisha nidhamu hii kwa msaada kwa wasomi wa Magharibi.

Wakati wa kuishi kwangu mjini London, niliombwa nifundishe kitabu *Mabaadii Usuul al-Fiqh* (cha Kiarabu) cha Sheikh Dr. Abd al-Hadi al-Fadhl kwa wanafunzi wanaozungumza Kiingereza katika Taasisi ya Imam Husein. Pale nilipata matatizo katika kutoa maelezo ya kimaalumati na mawazo ya kina ya kitabu *Usuul al-Fiqh* kwa Kiingereza. Pia nilishuhudia yale matatizo ambayo wanafunzi walikuwa nayo katika kuugundua *ulimwengu huu mpya*. Baada ya kumalizika kwa kozi hiyo niliombwa na taasisi hiyo kuandika kitabu cha kiada juu ya somo hilo hilo kwa lugha ya Kiingereza. Kile kitabu cha asili, yaani *Mabaadii Usuul al-Fiqh* kilikuwa kichukuliwe kama mfano katika ile namna ambayo mwandishi wake msomi huyu ameyaelezea mas'ala hayo kwa maelezo mepesi na mtiririko ya kimantiki na mpangilio wa masomo. Hata hivyo, niliamini kwamba haitatosha kutafsiri tu kitabu hicho kwa lugha ya Kiingereza. Njia ya kati na kati ilichaguliwa na hiyo ilikuwa ni kukitumia kitabu hicho cha Kiarabu kama msingi kwa ajili ya kitabu cha Kiingereza bila ya kulazimika kukifuata chote kwa ukamilifu wake. Mabadiliko mengi, uachaji na uongezaji umefanyika. Hata hivyo ule muundo wa kawaida wa maandishi ya asili umehifadhiwa. Hivyo mwandishi anahisi kwa ukweli kabisa kuwa mwenye deni kwa Dr. al-Fadhl, lakini huyo mwandishi mwenyewe anawajibika kikamilifu juu ya yaliyomo na vile vile hiyo lugha ya kitabu. Wasomaji wanaombwa kuchangia maoni yao



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 4 9/9/2015 12:56:01 PM

kuhusu kitabu hiki pamoja na mtunzi na kutoa mapendekezo yao kwa ajili ya uboreshaji wake.

Kitabu hiki kinakuja katika masomo kumi na mbili na kimeandaliwa kuwa kama kitabu cha utangulizi kwenye sayansi za *Usuul al-Fiqh*. Juhudi zinafanywa za kuyafanya mawazo hayo kuwa rahisi na wazi kwa kiasi iwezekanavyo bila ya kuhitajia elimu yoyote ya awali ya msomaji kuhusu somo hilo. Inatarajiwa kwamba kinaweza pia kuwa na msaada kwa wasiokuwa Waislam ambao wako tayari kujua zaidi kuhusu Uislam na hususan kuhusu namna ambavyo wanachuoni wa Fiqhi wa Shi'ah wanavyofikia hukumu za kiutendaji kutoka kwenye vyanzo vyao.

Sina budi hapa kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kukamilika kitabu hiki na ninaomba kwa moyo wote kwamba kiwe ni chenye manufaa kwa wale wanaotafuta elimu. Sina budi pia kuwashukuru wale wote ambao wameusoma muswada wa kitabu hiki na wakatoa maoni yenye thamani kubwa, hususan Abbas na Masumah Jaffer.

**Muhammad Ali Shomali**
**Rabi'al-Awwal, 1425, April 2004**

# SOMO LA KWANZA

## MISINGI YA SHARIAH (*FIQHI*)

**Ufafanuzi: Misingi** ya Shariah (Usuul al-Fiqh) ni elimu ya sheria za ung'amuzi wa hukumu za kisheria za Kiislam kutoka kwenye vyanzo vyake.[1]

**Ubainishaji wa ziada:** Kuna istilahi tatu kuu katika maelezo hayo hapo juu ambazo zinahitajia maelezo ya ziada:

1. Kanuni (*qaa'idah*)
2. Hukumu (*hukm*)
3. Chanzo (*daliil*)

**Kanuni**

**Ufafanuzi:** Kanuni ni tamko la kawaida la jumla ambalo linatumiwa kwenye mas'ala moja moja (maelezo) ili kupata hukumu zinazotokana nayo.

**Ufafanuzi wa ziada:** Ili kuweza kuelewa zaidi maana ya "kanuni" hiyo na njia za kufikia hukumu moja moja kutokana nayo tunatoa mfano ufuatao:

- Kanuni ya jumla: Kila maana ya dhahiri ya Qur'ani ni ushahidi sahihi na halali.
- Mas'ala moja moja: Ile aya ya Qur'ani, **"Na simamisheni Swala"** ambayo maana yake ya dhahiri ni wajibu wa mtu kutekeleza swala yake.

---

[1] Misingi ya shari'ah inaweza kuchukuliwa kama ndio utaratibu – methodolojia ya fiqhi.



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 6 9/9/2015 12:56:01 PM

- Matumizi: Matumizi yanaundwa kwa utaratibu upatikanao kutokana na fasili (ambao ni namna ya hitimisho la kimantiki juu ya hoja mbili) kwa namna ifuatayo:

**"Simamisheni" ni amri ya kawaida, na amri zote za kawaida ni dhahiri kwamba zinaashiria wajibu, kwa hiyo "Simamisheni" hii inaashiria wajibu.[2] Na kwa vile: "Simamisheni" inawakilisha maana ya dhahiri ya Qur'ani, na maana zote za Qur'ani ambazo ni za dhahiri ni ushahidi halali; kwa hiyo hatimaye tunafikia uamuzi kwamba hii aya ya "Simamisheni swala" ni ushahidi halali juu ya wajibu wa swala.**

**Hukumu – Maelezo:** Hukumu ni utoaji wa sheria kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kurekebisha na kuongoza maisha ya mwanadamu kuelekea kwenye ukamilifu katika kila nyanja.

**Ufafanuzi wa ziada:** Mwanadamu anaishi katika ulimwengu huu, na anaingiliana na kila anachokutana nacho katika maisha yake, na yapo mahusiano mbalimbali kati ya mja na Muumba Wake, kati ya watu wengine na yeye binafsi, kati ya mtu na mtu, ikiwa ni pamoja na familia yake mtu, jumuiya na ummah na baina ya mwanadamu na viumbe vingine, vyenye uhai na visivyo na uhai vyote. Maamiliano yote haya yanahitajia utaratibu na marekebisho kwa njia ya kuweka maelekezo kwa ajili ya kuongoza mwenendo wa mwanadamu. Hivi ni ili kwamba kila mahusiano ya mwanadamu, yawe ya kibinafsi, kifamilia, kijumuiya au kitaifa, hatimaye yamwongoze kwenye furaha na ustawi.

Sheria zilizotungwa ambazo zimeweka mfumo wa kuelekeza mwenendo wa kitabia wa mwanadamu ndio "hukumu" na hizi hukumu za kisheria za Kiislam zinazingira nyanja zote za mwenendo wa binadamu katika ulimwengu huu.

---

[2] Kuwa kawaida maana yake ni kuwa huru kutokana na ushahidi wowote muhimu ambao unaweza ukaainisha vinginevyo.



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 7 9/9/2015 12:56:01 PM

Kwa hiyo utungaji sheria wa Kiislam unaingiza maagizo maalum kwa ajili ya mwongozo wa mwanadamu katika nyanja zote za mwenendo wa binadamu, uwe wa mmoja mmoja au wa kijamii, na idadi ya maagizo haya ambayo yamewekwa ili kuelekeza tabia ya mwanadamu yanaitwa "Shariah;" kanuni ya sheria ya Kiislam.

**Aina za Hukumu:**

Hukumu inaweza kuwa ni moja kati ya namna mbili:

- Hukumu Halisi (*al-hukm al-waaqi'i*)
- Hukumu ya Wazi (*al-hukm al-dhaahiri*)

**Hukumu Halisi:** Hii ni ile hukumu iliyowekwa kwa ajili ya jambo katika uhalisia wake. Hukumu halisi badala yake zimegawanywa katika *hukumu halisi za msingi* na *hukumu halisi za hatua ya pili (secondary Rulings)*.

Kwa mfano: Tunahitaji Udhu kwa ajili ya swala, kwa hiyo bila udhu hatuwezi kuswali – hii ni hukumu halisi, ina uhalisia ambao hauwezi kupuuzwa.

Hukumu halisi ya msingi ni hukumu iliyowekwa kwa ajili ya jambo la peke yake, yaani ni kusema, bila ya kuzingatia vipengele vingine muhimu vya nje. Mifano ya aina hii ya hukumu ni: uruhusiwaji wa kunywa maji au wajibu wa kuchukua udhu kwa ajili ya swala.

Hukumu halisi za hatua ya pili ni hukumu zilizowekwa kwa ajili ya hali zisizo za kawaida, yaani ni kusema, ni panapokuwa na kipengele muhimu zaidi ambacho kinajuzu mabadiliko kwenye hukumu ya msingi juu ya jambo fulani. Kwa mfano, maji kwa kawaida yanaruhusiwa kunywa (unapojisikia), lakini inakuwa ni wajibu (wa lazima) wakati kama kuokoa maisha ya mtu kunategemea juu ya hilo. Hivyo hapa ile hukumu halisi ya msingi



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 8 9/9/2015 12:56:01 PM

– uruhusiwaji wa kunywa maji – inabadilika na kuwa hukumu ya hatua ya pili (*secondary ruling*) – yaani wajibu wa kufanya hivyo. Mfano mwingine: wakati kukiwa hakuna maji kwa ajili ya udhu wa swala zetu, inatubidi tufanya udhu huo kwa kutumia njia nyingine mbadala (*tayammum*).

**Hukumu ya Wazi:** Hii ni hukumu ambayo imewekwa kwa ajili ya jambo ambalo hukumu yake halisi haijulikani. Kwa mfano, tumechukua udhu wakati wa asubuhi lakini unapofika wakati wa swala ya mchana tunakuwa hatuna uhakika kama ule udhu bado upo na ni thabiti. Kwa kawaida tunakuwa na shaka juu ya udhu huo kwa uhakika. Hata hivyo, kwa desturi tunaweza tukachukulia kwamba udhu huo bado upo na una athari, labda kama tukiwa na ushahidi unaoashiria vinginevyo. Hii haiashirii uhakika bali ni wazo la kidesturi tu.

**Chanzo:** Kama tulivyoona mapema, misingi ya fiqhi inatufundisha zile kanuni za maamuzi ya hukumu za kisheria za Kiislam kutoka kwenye vyanzo vya sheria za kimungu (*Shariah*). Hivyo dalili ndio msingi ambao kwamba hukumu za Kiislam zinaweza kufikiwa. Hivyo wanachuoni wa Kishiah kwa kawaida wanavihesabu vitu vinne kama ndio vyanzo vya asili au vya msingi kabisa vya sheria ya Kiislam, ambavyo kutoka humo hukumu moja moja zinaweza kufikiwa. Vyanzo hivyo vinne (al-Adillat al-arba'ah) vinakuwa ni:

1. Qur'ani Tukufu
2. Sunnah – maneno, vitendo na aliyonyamazia kimya Mtume (s.a.w.w.)
3. Akili



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 9 9/9/2015 12:56:01 PM

4. Makubaliano (*Ijmai*) [3]

**Angalizo:** Ushahidi ambao unaweza kupatikana katika kila kimojawapo cha vyanzo hivyo hapo juu kinaweza kurejelea kwenye hukumu halisi (*al-hukm al-waaqi'i*). Ushahidi kama huo unaitwa dalili (*al-daliil al-ijtihaadi*). Ushahidi unaorejelea kwenye hukumu ya wazi (*al-Hukm al-dhaahirii*) unaitwa "*al-daliil al-fiqaahiy*." Kuna aina nne za *al-daliil al-fiqaahiy*: *al-baraa'ah, al-istishab, al-takhyiir* na *al-ihtiiyaat*.[4]

**Maudhui ya Misingi ya Shariah:**

Wanachuoni wengi wanakubali kwamba kila elimu ina maudhui yake ambayo inaunganisha vipengele vyote vya elimu hiyo. Kwa mfano maudhui ya elimu ya matibabu ni mwili wa mwanadamu. Nini maudhui ya kanuni za fiqhi? Maoni maarufu ni kwamba maudhui ya misingi ya fiqhi ni hivyo vyanzo vinne vya hukumu za kidini, lakini ni kiasi uamuzi wa hukumu za kidini unavyohusika. Hivyo mijadala mingi kuhusu elimu za Qur'ani au hadithi au akili ambayo haiendani na mchakato wa uamuzi wa hukumu za kidini haichukuliwi, inaachwa.

**Faida ya Misingi ya Shariah**

Faida ya kujifunza elimu ya misingi ya sheria ni kupata uwezo wa kufikia hukumu za kidini kutoka kwenye vyanzo vyake, yaani kuwezeshwa kuwa na uelewa asilia wa sheria za Kiislam.

---

[3] Haya yataelezewa kwa kina zaidi katika milango inayofuatia

[4] Kanuni zote hizi nne zinazungumzia kile ambacho ni lazima kifanyike kwa vitendo iwapo kama hakuna njia ya kufahamu ile hukumu ya kweli. Kwa hiyo hizi nne zinaitwa pia "al-usuul al-amaliiyah" au "Kanuni ya kimatendo" Al-bara'ah inahitajia kuchukulia kwamba hakuna wajibu. Al-istishaab inahitajia kwamba uchukulie muendelezo wa ile hukumu ya awali iliyothibiti. Al-takhyuu inahitajia kwamba uchukulie kuwa na fursa kati ya uwezekano badali mbili na al-ihtiyaat inahitajia tahadhari. Maelezo na masharti ya mambo manne haya yatachunguzwa katika Somo la Kumi na moja.



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 10 9/9/2015 12:56:01 PM

# SOMO LA PILI

## MGAWANYIKO WA HUKUMU

Hukumu, ziwe halisi ama za dhahiri zimegawanyika kwenye:

- Hukumu ya Wajibu wa Jumla (*al-hukm al-takliifiy* - الحكم التكليفي )

- Hukumu ya Hali (*al-hukm al-wad'iy* - الحكم الوضعي )

**Hukumu ya Wajibu wa Jumla:** Hizi ni zile hukumu ambazo zinafungamana na vitendo vya mwanadamu na zinashughulika moja kwa moja na tabia ya mwanadamu katika vipengele mbalimbali vya maisha yake. Hukumu hizi zinajumuisha pamoja na uharamu wa kunywa vinywaji vyenye vileo, wajibu wa kuwasaidia kifedha ndugu fulani wa karibu na ruhusa ya kunywa maji. Hukumu za wajibu wa jumla hatimae zinagawanyika mafungu matano:

1. **Wajibu (al-wujuub - الوجوب ):** Hii ina maana kwamba kitendo fulani kinalazimishwa na tunawajibika kukitenda na hatuna chaguo jingine katika suala hilo. Kutenda kitendo hicho kunastahiki thawabu, na kama hatukukifanya basi tunastahili kuadhibiwa.

2. **Iliyopendekezwa – Mustahabu (al-Istihbaab – الاستحباب an-Nadb– الندب ):** Hii ina maana kwamba kitendo fulani kimependekezwa kufanyika lakini tuna fursa ya chaguo. Kufanya kitendo hicho kunastahiki thawabu, bali kama hatutakifanya hatustahili adhabu.



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 11 9/9/2015 12:56:01 PM

3. **Haramu (*al-hurmah* – الحرمة):** Hii ina maana kwamba kitendo fulani kimekatazwa yaani kimeharamishwa kufanyika na hatuna hiari katika suala hilo. Kujizuia na kitendo hicho kunastahiki thawabu, lakini endapo kama tutakifanya basi tutakuwa tunastahili kuadhibiwa.

4. **Makruhu (*al-karaahah* – الكراهة):** Hii maana yake ni kwamba kitendo fulani kimewekewa kikwazo kufanyika kwake, lakini tunayo fursa ya hiari. Kujizuia na kitendo hicho kunaleta thawabu, lakini kama tukikifanya basi hatuwajibiki kuadhibiwa.

5. **Mubaha – Kukubalika (*al-ibaahah* – الأباحة):** Maana yake ni kwamba kitendo fulani hakikufungika. Hakuna maelekezo maalum yaliyowekwa na sheria, na hivyo hakuna thawabu au adhabu iliyohusishwa juu yake.

**Hukumu ya Kimazingira:** Hii ni hukumu ambayo kimsingi hauhusiani na vitendo vyenyewe bali inatunga sheria juu ya hali fulani fulani au mahusiano ambayo yanaathiri mwenendo wa mwanadamu kwa njia isiyo ya moja kwa moja, kama vile hukumu za ndoa ambazo zinawekea sheria uhusiano makhsusi baina ya wanaume na wanawake kwa namna ya moja kwa moja, lakini zinaathiri na kurekebisha mwenendo wa mwanadamu kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Kwa maneno mengine hukumu za ndoa zinawekea sheria uhusiano ambao kwa namna isiyo ya moja kwa moja zinaashiria wajibu fulani wa kivitendo, kama vile majukumu ya mume kuhusu mke wake na kinyume chake.[5]

[5] Hukumu za kimazingira zinaweza kuamua hali kama ndoa, talaka na unajisi wa damu au uhusiano wa kati ya kitendo na athari yake kama vile adhabu kwa ajili ya wizi au uhusiano chanya kati ya jambo na shuruti zake, kama vile swala na udhuu au uhusiano hasi, kama ule kati ya urithi na mauaji, kwa vile mtoto anayewauwa wazazi wake hawezi kurithi kutoka kwao.



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 12 9/9/2015 12:56:01 PM

**Upambanuzi wa Wajibu** [6]

Wajib unaweza ukapambanuliwa katika idadi ya njia mbili:

**1.** Wajibu binafsi dhidi ya wajibu wa pamoja

Upambanuzi huu umeegemea juu ya iwapo wajibu huo unamzungumzia kila mtu mmoja mmoja binafsi yake kama vile hizi swala za kila siku, au unazungumzia Waislam wote kwa jumla, kama vile ule wajibu wa kumzika aliyefariki. Katika suala la wajibu binafsi, kila mtu anawajibika, na utendaji wa mtu wa kitendo hicho hautoshelezi kwa wengine. Hata hivyo katika suala la wajibu wa pamoja jamii inawajibishwa. Kwa hiyo utekelezaji wa kitendo hicho wa mtu mmoja unatosheleza na kwa wengine pia, lakini kama tendo hilo halitafanyika, basi watu wote wanawajibika na wanastahili kuadhibiwa.

Istilahi za kimaalumati kwa wajibu binafsi ni *al-wuujuub al'ayni* na kwa wajibu wa pamoja ni *al-wuujuub al-kifaaiy*. Kwa hiyo kitendo cha wajibu binafsi kinaitwa "*al-wajib al-'ayniy*" (الواجب العينى) na kitendo cha wajibu wa pamoja kinaitwa "*al-waajib al-kifaaiy*" (الواجب الكفائي).[7]

**2.** Wajibu bila fursa ya chaguo dhidi ya wajibu wenye fursa ya chaguo.

Upambanuzi huu umeegemea juu ya iwapo wajibu huo ni wa kwenye kitendo ambacho hakina mbadala au cha kupokezana nacho kama kufunga katika mwezi wa Ramadhani, au unakuwa

---

[6] Inapasa kuzingatiwa kwamba wajibu ni kile kitendo ambacho ni cha lazima na wajibu ndio ulazima wenyewe.

[7] Hivyo, al-waajib al-'ayniy unarejelea kwa wajibu wa watu wote na unampasisha kila mmoja kwa mfano, hizi swala tano ambapo al-waajib al-kifaaiy unarejelea kwenye wajibu wa watu wote lakini hauhusiki kwa watu wote iwapo kama mtu mmoja atachukua jukumu la kuutenda – kwa mfano kuizika maiti ya Muislam aliyefariki.



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 13 9/9/2015 12:56:01 PM

ni wa kwenye kitendo ambacho kinaweza kufanyiwa mbadala na mwingine kama Swala ya Ijumaa ambayo inaweza kuchukuliwa zamu mbadala na swala ya Adhuhuri. [8]

Istilahi ya kimaalumati kwa ajili ya wajibu usio na hiari ni *al-wujuub al-ta'yiinii* na kwa ajili ya wajibu wenye fursa ni al-wuujuub al-takhyiiri. Kwa hiyo kitendo cha wajibu kisicho na mbadala kinaitwa "*al-waajib al-ta'yiinii*" (الواجب التعينى) na kile kitendo cha wajibu wenye fursa ya chaguo unaitwa "*al-waajib al-takhyiirii*" (الواجب التخيرى).

## 3. Wajibu wenye wakati dhidi ya wajibu usio na wakati.

Upambanuzi huu umeegemea juu ya iwapo kitendo hicho cha wajibu kimeegemea kwenye wakati (au wa wakati) kama ule wajibu wa swala tano za kila siku na kwenda Hijja huko Makka au sio kama wajibu wa kuamrisha mema na kukataza maovu (*al-amr bi al-ma'ruuf na al-nahy 'an al-munkar*).

Istilahi ya kimaalumati kwa ajili ya wajibu ulioko kwenye kitendo kinachotegemea wakati ni *al-wuujuub al-muwaqqat* ( الوجوب الموقت ) na wajibu ulioko kwenye kitendo ambacho hakitegemei kwenye wakati ni *al-wujuub ghayr al-muwaqqat* (الوجوب غير الموقت). Kwa mfuatano vitendo hivi vinaitwa "*al-waajib al-muwaqqat*" na "*al-waajib ghayr al-muwaqqat.*"

*Al-waajib al-muwaqqat* unaweza kugawanyika zaidi kwenye *al-muwaqqat al-mudhwayyaq* (الموقت المضيق) na *al-muwaqqat al-muwassaa* (الموقت الموسع). *Al-muwaqqat al-mudhwayyaq* inarejelea vitendo ambavyo vinadumu kwa muda wote viliopangiwa kufanyika

8 Baadhi ya mafaqihi wanaamini kwamba katika kipindi hiki cha ghaibu ya Imam Mahdi (a.t.f.s.) watu wana fursa ya kuchagua mnamo siku ya Ijumaa kuswali ama swala ya Ijumaa yenye rakaa mbili na hotuba mbili zitolewazo na Imam wa Ijumaa au kuswali swali ya kawaida ya Adhuhuri yenye rakaa nne.



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 14 9/9/2015 12:56:01 PM

kama vile saumu ambayo inadumu kuanzia alfajiri mpaka kuzama kwa jua wakati wa magharibi. *Al-muwaqqat al-muwassaa* unarejelea kwenye vitendo ambavyo vinadumu kwa kiasi tu cha wakati wote uliopangwa kwa ajili ya utendaji wake kama vile swala za kila siku.

## 4. Wajibu wa jumla dhidi ya wajibu wenye shuruti.

Upambanuzi huu umetegemea juu ya iwapo wajibu huo ni wa jumla na usio na mipaka kama swala tano za kila siku ambazo ni wajibu katika mazingira yote, au ni wenye shuruti kama wajibu wa kwenda kuhiji Makka ambako kunategemea juu ya kukamilisha na kumudu masharti fulani.

Istilahi za kimaalumati kwa ajili ya huo wajibu wa jumla ni *al-wuujuub al-mutlaq* (الوجوب المطلق) na kwa wajibu wenye shuruti ni *al-wujuub al-muqayyad* (الوجوب المقيد) au *al-wujuub al-mashruut*.

*Al-wujuub al-mutlaq* unaweza kugawanyika zaidi katika ule wa kutimiza (*al-munajjaz* – المنجز) na ule wa kutegemea hali fulani (*al-mu'allaq* – المعلق) huo uliyotangulia unarejelea kwenye wajibu ambao upo hadhir na ukifanya kazi, kama ule wajibu wa kuswali swala ya Dhuhr pale wakati wake unapokuwa umeingia tayari. Na huu mwingine unaofuatia unarejelea kwenye wajibu ambao umeandikwa kama vile wajibu wa kuswali swala kabla ya wakati wake kuingia.

## 5. Wajibu wa kiibada dhidi ya wajibu usio wa kiibada

Upambanuzi huu umetegemea iwapo wajibu huo unahitajia kitendo cha kiibada ama hapana. Vitendo vya kiibada kama vile swala na saumu vinalazimu niya ya kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu. Vitendo visivyo vya kiibada, kama vile mtu kufua nguo yake iliyonajisika ama kuufanya msikiti kuwa tohara baada ya kuwa umechafuka hakuhitaji niya yoyote maalum ili kuwa halali.



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 15 9/9/2015 12:56:01 PM

Istilahi ya kimaalumati kwa ajili ya wajibu wa kiibada ni *al-wujuub al-ta'abbudii* ( الوجوب التعبدى ) na kwa wajibu usio wa kiibada ni *al-wujuub al-tawassuliiy* ( الوجوب التوصَلى ).

**6.** Wajibu wa kiasi – kiidadi dhidi ya wajibu usio wa kiasi

Upambanuzi huu unategemea iwapo kitendo cha wajibu kimeainishwa kwa kiasi chake na kufafanuliwa ama laa. Mfano mmoja wa wajibu wa kiasi ni hizi swala tano ambamo kiasi kimeainishwa kwa uwazi, yaani rakaa mbili kwa ajili ya swala ya Fajr, rakaa nne kwa ajili ya swala ya Dhuhr, nne kwa swala ya Asri, rakaa tatu kwa ajili ya swala ya Maghribi na rakaa nne kwa ajili ya swala ya Isha'. Huo wajibu usio wa kiasi ni kama ule wajibu wa kuwa mwadilifu na mkarimu ambao hauna kiasi wala mipaka.

Istihali ya kimaalumati ya wajibu wa kiasi ni *al-wujuub al-muhaddad* (الوجوب المحدّد) na ya wajibu usio na kiasi ni *al-wujuub ghayr al-muhaddad* (الوجوب غير المحدّد)**.**



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 16 9/9/2015 12:56:01 PM

# SOMO LA TATU

## VYANZO VYA REJEA

### QUR'ANI TUKUFU

Kwa hakika Qur'ani Tukufu ndio chanzo cha kwanza na cha muhimu sana cha Uislam kwa jumla na cha hukumu za Kiislam kwa umakhsusia.

**Ufafanuzi:** Qur'ani ni "Kitabu" (al-Kitab – الكتاب), kilichoteremshwa na Mwenyezi Mungu swt. kwa Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.) na kitabu hicho ndicho kinachochukuliwa kama Qur'ani. Haya maneno "ndicho kinachochukuliwa kama Qur'ani" ni kwa ajili ya kuondoa zile semi Tukufu, kwa vile hazichukuliwi kama ni sehemu ya Qur'ani, ingawa nazo zimeteremka kutoka kwa Mwenyezi Mungu pia.[9] Maneno haya pia yanaondoa zile hadithi za Bwana Mtume (s.a.w.w.) kwa vile hazichukuliwi kama ni sehemu ya Qur'ani, ingawa "Mtume yeye hazungumzi kamwe kutokana na matakwa yake, si chochote bali ni wahyi uliofunuliwa kwake."[10]

Ufafanuzi huo hapo juu unaonyesha kwamba si chochote

[9] Semi Tukufu (al-hadithi al-qudsiiy –الحديث القدسى) ni maneno ya Mwenyezi Mungu kwa ulimi wa Mtukufu Mtume. Kwa maneno mengine, katika suala la hadithi al-qudsiy maana zake zinafunuliwa kwa mitume, lakini maneno yenyewe yanatoka kwa mitume wenyewe. Yaani, hao mitume wanapokea maana zenyewe kutoka kwa Mwenyezi Mungu na kisha wao wanawaeleza watu kwa maneno yao wenyewe. Kwa hiyo hadithi hizo Tukufu zilizoteremshwa kwa Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.) hazichukuliwi kama ni sehemu ya Qur'ani.

[10] Surat an-Najm; 53:3



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 17 9/9/2015 12:56:01 PM

isipokuwa ile Qur'ani ya Kiarabu ya asili ambayo tunayo leo hii ndio Qur'ani. Kwa hiyo, hakuna tafsiri au tarjuma ya Qur'ani inayoweza kuchukuliwa kama Qur'ani kwani sio neno la Mwenyezi Mungu kamwe.

Kuna makubaliano ya pamoja miongoni mwa Waislam kwamba Qur'ani tuliyonayo mikononi mwetu leo hii ni Qur'ani ile ile iliyokuwa imeteremshwa kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hakuna chochote kilichoongezwa au kilichoondolewa.[11] Qur'ani imesimuliwa na idadi kubwa ya watu katika kila kizazi (*al-tawaatur* – التواتر) na kwa hiyo hakuna nafasi ya uharibifu wowote kuweza kuwa umepenyeza kwenye maandishi yake hayo.

Kuna riwaya nyingi sana kutoka kwa Maimam wa Ahlul-Bayt (a.s.) zinazolithibitisha jambo hili. Kwa kweli kwa mujibu wa maelekezo yaliyotolewa na Maiman hawa, njia mojawapo ya kuthibitisha hadithi zilizosimuliwa kutoka kwao ni kuona kwamba zinakubaliana na Qur'ani ama laa. Hivyo "Kama ukiona hadithi yoyote isiyoendana na Qur'ani basi hiyo uiache kabisa.

Ndani ya Qur'ani masuala mengi mbalimbali yametajwa, lakini takriban aya 500 (kama 1/3) za Qur'ani zinahusika na sheria za kimatendo na hukumu za Shariah. Hizi zinajulikana kama *Aayaat al-ahkaam* (ايات الاحكام).

**Uhalali wa Qur'ani:** Kama ilivyosemwa kabla, hakuna shaka miongoni mwa Waislam kwamba Qur'ani hii hii ambayo inapatikana leo ilishuka kwa Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.) kama mwongozo wa kudumu kwa ajili ya mwanadamu. Kwa hiyo hakuna mabishano kuhusiana na usahihi na uhalali wa Qur'ani. Chochote mtu anachoweza kukielewa vizuri na kwa uhakika zaidi kutoka ndani ya Qur'ani ni sahihi na inaweza kuchukuliwa kama ushahidi

[11] Tazama Surat Yunus; 20:37



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 18 9/9/2015 12:56:01 PM

katika kufafanua kile kilicho cha kweli au ambacho Mwenyezi Mungu ametutaka sisi tukifanye. Hiki ndicho tunachomaanisha kwa Qur'ani kuwa ni chanzo.[12]

## SUNNAH

**Ufafanuzi:** Sunnah inakuwa ni katika kauli (القول), vitendo (الفعل), na kukubali jambo kwa kulinyamazia kimya (التقرير) kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

Al-Marhum Shaahid al-Mutahhari anasema:

> "Ni dhahiri kabisa, kama Mtukufu Mtume alielezea sheria fulani kwa maneno, au kama inajulikana jinsi Mtume alivyotenda wajibu fulani wa kidini, au kama

[12] Kumekuwa na kikundi kidogo cha wanachuoni ambao waliamini kwamba haiwezekani kwa sisi kufikia hukumu ya Kiislam kutoka kwenye Qur'ani yenyewe, kwa sababu aya za Qur'ani zina kina kikubwa katika maana zake na mara kwa mara zinawasilisha uwezekano mbali mbali. Hivyo, kimsingi wao wanaamini kwamba haiwezekani kufikia fatwa za Kiislam kutoka ndani ya Qur'ani bila ya muongozo wa Sunnah. Hata hivyo, hii haina maana kwamba Qur'ani sio chanzo sahihi, bali ina maana kwamba uelewa wetu wa Qur'ani unahitajia kuongozwa.
Bila shaka, maoni haya hayapatani na mafundisho ya Mtume na Maimam (a.s.) ambao wametutaka sisi tuzihakiki hadithi zilizosimuliwa kutoka kwao kwa kipimo cha Qur'ani. Kwa mfano, Ibn Abii Ya'fuur anasema: "Nilimuuliza Abuu Abdillah (Imam Sadiq) kuhusu hadithi mbalimbali zinazosimuliwa na wale ambao tunawaamini na pia kutoka kwa wale ambao hatuwaamini. Alipoyasikia haya, Imam alijibu: "Wakati wowote unapopokea riwaya ambayo imevuliwa na aya yoyote kutoka kwenye Kitabu cha Mwenyezi Mungu au hadithi ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) iliyothubutu, basi ikubali. Vinginevyo riwaya hiyo iachwe kwa ajili ya huyo tu ambaye ameileta kwako," (*Usuul al-Kafi*, toleo la Kiarabu-Kiingereza, Riwaya ya 202).
Vilevile kuna hadithi ambamo Maimam wanasema "Chochote tunachowaambieni, mtuulize rejea zake kwenye Qur'ani." Kwa mfano, wakati Imam as-Sadiq (a.s.) alipoulizwa alivyokuwa anajua kwamba kupaka – mash ya kichwa ilikuwa ni kupaka sehemu ya kichwa yeye alisema ilikuwa ni kwa sababu ya neno 'bi' lililotumika kwenye aya ya udhuu.



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 19 9/9/2015 12:56:02 PM

> inajulikana kwamba wengine walifanya wajibu fulani wa kidini mbele yake katika namna fulani ambayo ilipata baraka zake na idhini – kunyamaza kwake kunaashiria kukubali kwake – hii inatosha kuwa ni ushahidi (dalil) kwa faqih kulichukulia tendo hilo kuwa sheria halisi ya Kiislam.[13]

**Uhalali wa Sunnah:** Hakuna shaka miongoni mwa Waislam kwamba baada ya Qur'ani Tukufu Sunnah ya Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.) ndio chanzo muhimu sana kwa ajili ya kuuelewa Uislam, ikiwa ni pamoja na sheria za Kiislam (*Shariah*). Kwa kweli inaelekea kuwa ni wazo la wote miongoni mwa watu wa dini tofauti, mataifa na tamaduni zote kwamba chanzo salama na cha kutegemewa kwa ajili ya kuelewa dini yoyote au madhehebu ni kurejea kwa mwanzilishi wake au mtu aliyeteuliwa na mwanzilishi huyo kuitambulisha na kuiwasilisha dini au madhehebu hiyo kwa watu.

Qur'ani Tukufu inatoa kwa uwazi kabisa cheo cha hali ya juu kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Yeye Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ndiye mtu mwenye wajibu wa kuielezea Qur'ani (16:44) na kufundisha Qur'ani na hekima (62:2), Mtume ni kigezo bora kwa waumini (33:21), ambaye kamwe hazungumzi kwa matamanio yake (53:3). Qur'ani pia inawataka Waislam kushikamana na kile anachowapa na kujizuia na kile anachowakataza (59:7).

## Watu wa Nyumba ya Mtume:

Kwa mujibu wa hadithi sahihi na za wazi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) zinazosimuliwa na wote Sunni na Shi'ah, Waislam wanaambiwa warejee kwenye mafundisho ya watu wa Nyumba ya

---

[13] Murtadha Mutahhari, *Understanding Islamic Sciences* (London, ICAS, 2002)

Mtume (*Ahlul-Bayt* – اهل البيت) ili kupata uelewa salama salimini juu ya Uislam.[14]

Mojawapo ya hadithi ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuhusiana na hili ni ile hadithi mashuhuri ya *Thaqalayn* (حديث الثقلين):

**"Enyi watu! Mimi ninaacha miongoni mwenu vizito viwili vyenye thamani: Kitabu cha Mwenyezi Mungu na watu wa nyumbani kwangu. Pindi mtakapokuwa mmeshikamana navyo viwili hivyo hamtopotea kamwe,"**

Ama katika riwaya nyingine Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) amesema:

> "Nawaachieni miongoni mwenu vitu viwili ambavyo kama mtashikamana navyo hamtapotea kamwe baada yangu: Kitabu cha Allah ambacho ni kama kamba iliyonyooshwa baina ya mbingu na ardhi, na kizazi changu, na viwili hivi havitatengana mpaka vinifikie kwenye haudhi Siku ya Kiyama. Tazameni na kuweni waangalifu juu ya jinsi mtakavyoshughulika navyo baada yangu."

Riwaya hizo hapo juu zinaweza kupatikana katika vyanzo vikuu vya Sunni kama vile *Sahih Muslim*, Jz. 8, uk. 25 hadithi ya 2408; *Musnad Ahmad Ibn Hanbal* Jz. 3, uk.388 hadithi ya 10720; *Sunnan Daarimii* Jz. 2, uk. 432; *Sahih at-Tirmidhii* Jz. 5, uk. 6432 hadithi ya 3788. Zimetajwa pia katika vitabu kama *Usd al-Ghaabah* cha Ibn al-Athiir Jz. 2, uk.13; *Sunan al-Kubraa* ya Bayhaqii Jz. 2, uk. 198 na *Kanz al-Ummaal* cha Muttaqii al-Hindii Jz. 1, uk. 44.

---

[14] Kwa maelezo ya kina zaidi juu ya Sunnah, tazama: *Discovering Shi'i Islam* (Qum, Jami'at al-Zahra, 2003) uk. 33



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 21 9/9/2015 12:56:02 PM

**Jinsi gani ya kuhakiki hadithi inayotajwa?**

Kabla ya kufikia hukumu ya Kiislam yoyote ile kutoka kwenye hadithi iliyotajwa, mtu hana budi kuhakikisha usahihi wa hadithi hiyo na hili linafanyika kwa kuchunguza nyororo ya wasimuliaji (*al-sanad* – السند). Ni baada tu ya kuwa hadithi imethibitishwa ndipo faqihi anapochunguza matini halisi (*al-matn* – المتن) ya hadithi hiyo. Hiyo kazi ya awali haihitajiki katika kufikia hukumu ya Kiislam kutoka kwenye Qur'ani, kwa vile hakuna shaka kwamba Qur'ani yote ni sahihi.

Hivyo kuhusiana na Qur'ani, huyo faqihi anahitaji tu kuhakikisha anao uelewa mzuri juu ya matini hiyo. Hata hivyo, kuhusiana na Sunnah, hanabudi kwanza kuhakikisha kwamba anayo riwaya ya kutegemewa hasa juu ya Sunnah hiyo na kisha aendelee kupata mafuhumu yake ya sawa.

Kwa nyongeza ya kwenye kanuni za kilugha zinazosomwa katika kanuni za fiqhi ambazo zinafafanua jinsi ya kuyaelewa maandisi ya Qur'ani na Sunnah, elimu mbili tofauti za *Diraayat al-Hadith*i na *Al-Rijaal* zimeendelezwa ili kumwezesha faqihi kuthibitisha na kuainisha riwaya ya mdomo au ya maandishi juu ya Sunnah. Kuweza kuelewa utaratibu wa namna ya kuelewa hadithi, mtu anapaswa kuzingatia maelezo yanayostahiki ya kanuni za fiqh, *Dirayaat ah-Hadith*i na *Al-Rijaal*.

Katika kile kinachofuata, ninarejea tu kwenye vile vipengele vya utaratibu huu. Kuwa na uwezo wa kutumia hadithi iliyotolewa kama rejea yake, mwanachuoni wa Ki-Shi'ah anachohitajia kwanza ni kuchunguza angalau mambo matatu;

**1.** Njia ambayo kwamba amepatia kitabu chenye hadithi hiyo. Kwa mfano, kama hadithi imetajwa katika *al-Kafi*, ambacho



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 22 9/9/2015 12:56:02 PM

kiliandikwa katika karne ya nne, mtafiti hana budi kuhakikisha kwamba hiyo nakala ya *al-Kafi* aliyonayo inafanana na ile nakala ya mwandishi. Kwa lengo hili wanachuoni wa hadithi wa Shi'ah, kizazi baada ya kizazi wamekuwa wakikagua nakala zao za vitabu hivyo wakiwa na mabwana wakubwa wao, hadithi baada ya hadithi, na wakiwa wamemaliza kazi hii ndipo wangepata ruhusa kutoka kwa mabwana zao ya kusimulia kutoka kwa mwandishi wa kitabu cha asili.

**2.** Baada ya kuhakikisha kwamba kile kitabu alichonacho mikononi mwake kinafanana na kitabu cha asili, mwanachuoni hana budi kuchunguza nyororo ya wasimuliaji wake ambao kupitia kwao ameipata hadithi hiyo kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) au Maimam (a.s). Kwa ajili ya lengo hilo anapaswa kuhakikisha hakuna kinachokosekana katika sanadi ya wasimulizi, kwamba wote wanaooneka katika sanad hiyo wanatambulishwa sawa sawa na hatimaye wale wanaotambulishwa kama wasimuliaji wanakuwa waaminifu na wa kutegemewa. Kama mtu mmoja kati ya kumi mathalani akikosekana, anakuwa hajulikani vema, au anajulikana kama ni muongo, basi sanadi yote inakuwa batili.

**3.** Wakati mambo mawili hayo ya kwanza yakisha kamilika, mwanachuoni wa hadithi lazima baada ya hapo afanye uchunguzi kadhaa wa jumla kuhusu yaliyomo kwenye hadithi hiyo ili kumuwezesha kuitumia hadithi hiyo kama rejea yake. La kwanza ni kuipima hadithi kama inaendana na Qur'ani au hapana. Bila ya shaka yoyote ile kwamba Mashi'ah wote wanakubaliana kwamba hadithi yoyote inayopingana na Qur'ani au inakwenda kinyume na mafundisho ya Qur'ani lazima ikataliwe, hata kama wasimuliaji wote wakawa ni waaminifu na wakutegeme-



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 23 9/9/2015 12:56:02 PM

wa. Kuna maelekezo ya wazi kutoka kwa Maimam wa Nyumba ya Mtukufu Mtuma (s.a.w.w.) kuhusiana na suala hilo.[15]

Kwa hiyo, Mashi'ah hawaamini juu ya mkusanyiko (kitabu cha hadithi za kweli tupu) unaoitwa *Sahiih.* Hata ile mikusanyiko mikubwa ya hadithi za wanachuoni wa Shi'ah, vitabu kama vile *al-Kafi, Man laa Yahdhuruhuu al-Faqiih, Tahdhiib al-Ahkaam* na *Al-Istibsaar* havichukuliwi na wakusanyaji wake wala na wanachuoni wengine kuwa viko mbali na kuweza kufanyiwa vipimo na utathmini.[16] Kila mojawapo ya hadithi iliyotajwa kwenye kitabu chochote chenye mkusanyiko wa hadithi ni lazima ichunguzwe peke yake. Ni Qur'ani pekee ambayo ndio Kitabu sahihi chote kwa ujumla wake na ambacho kwamba kila chanzo kingine lazima kiende kulingana nacho. Yule bingwa mkubwa wa hadithi, Sheika al-Kulayni, katika utangulizi wake kwenye *Usuul al-Kafi* anasema:

> "Ndugu, Mwenyezi Mungu akuongoze kwenye njia iliyonyooka. Huna budi kujua kwamba sio jambo la kila mmoja kuweza kupambanua ukweli katika hadithi zinazogongana zinazopatikana kutoka kwa Ulamaa hawa (Maimam) amani juu yao, isipokuwa kwa kupitia viwango vilivyotangazwa na al-Aalim (yaani Imam): Pima riwaya zinazogongana kwa kutumia Kitabu cha Allah, na ile ambayo inakubaliana nacho ichukueni, na ile inayopingana nacho, hiyo ikataeni.

[15] M.A. Shomali, *Shi'I Islam: origins, Faith and Practices*

[16] Kwa mfano, Muhammad Baqir al-Majlisii , mwanachuoni mashuhuri wa hadithi katika *Mir'aat al-Uquul* anatathmini hadithi za *al-Kafi* moja baada ya nyingine na anaelezea maoni yake binafsi kuhusiana na usahihi wake na yaliyomo kwenye maudhui zao.



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 24 9/9/2015 12:56:02 PM

# UPAMBANUZI WA HADITHI

Riwaya zinaweza kuanishwa kulingana na sanadi zao:

*1.* ***Al-khabar al-maqtuu' al-suduur*** (الخبر المقطوع الصدور) – hii ni riwaya ambayo hakuna shaka kwamba imesimuliwa na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) au Maimam (a.s.). Kundi hili linagawanyika zaidi namna mbili:

**1.1 al-Mutawaatir (المتواتر) –** hii ni riwaya ambayo imesimuliwa na idadi kubwa sana ya watu kiasi kwamba haiwezekani kukawa na shaka juu ya usahihi wa hadithi hiyo.

**Al-muqtarin bimaa yufiyd al-qat' (المقترن بما يفيد القطع)** hii ni riwaya ambayo inatoa uhakika kutokana na ushahidi mwingine. Kwa mfano, maudhui ya riwaya ni ya kiwango cha juu sana kiasi kwamba hakuwezi kuwa na shaka kwamba inatoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), au kwa Ahlul-Bayt wake (a.s.), kama ile *Ziarat al-jaami 'ah* (الزيارة الجامعة). Au riwaya iko kwa namna ambayo inazungumza dhidi ya wale walioko madarakani – itakuwa haiyumkiniki kabisa kwamba hadithi ya aina hiyo iwezekuwa imebuniwa kwa vile hakuna faida ndani yake kwa huyo mzushi.

**2. Al-khabar ghayr al-maqtuu' al-suduur**
**(الخبر غير المقطوع الصدور)** – hii ni riwaya ambayo hatuwezi kuwa na uhakika kama kweli imetoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kweli hasa au na Maimam(a.s.). Kundi hili pia linarejelewa kama *khabar al-waahid* (خبر الواحد)**.** Ingawa neno "waahid" kwa Kiarabu lina maana ya moja, kimaalumati haimaanishwi kurejea kwenye riwaya iliyosimuliwa na mtu mmoja. Inarejea kwa kila hadithi ambayo haiwezi kuainishwa chini ya mutawaatir na, zaidi ya hapo haina ushahidi



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 25 9/9/2015 12:56:02 PM

mwingine wowote wa kuthibitisha kwamba imetoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ama kwa Ahlul-Bayt wake (a.s.).

Kundi hili limegawanyika tena zaidi kwenye

**2.1 Al-musnad (المسند)** watu wote katika mnyororo wa wasimuliaji wametajwa kwa majina na kwa hiyo wanaweza kuchunguzwa, na hakuna mwanya katika silsila hiyo. Riwaya za Musnad zinaweza kuchukuliwa kama ni sahih baada tu ya uchunguzi zaidi juu ya wasimuliaji ambao wametokea kwenye silsila hiyo utakapofanyika, na hili linawezekana kwa sababu wasimuliaji wote wamekwisha kutajwa.[17]

**2.2 Mursali (*mursal* – المرسل )** – kuna mwanya ndani ya silsila. Halafu hadithi zinatajwa kulingana na udhaifu wake, katika utaratibu unaofuata:

**2.1.1. Sahihi (*sahih* – الصحيح )** – hii ni riwaya ambayo wapokezi wake wote ni Shi'ah na ni wakweli. Hadithi ya namna hii inachukuliwa kwamba ni sahihi na Wanachuoni wote.

**2.1.2. Inayotegemewa (*muwaththaq* – الموثق)** – hii ni riwaya ambayo wapokezi wake wote ni wakweli lakini sio lazima wawe Shi'ah. Aina hii ya riwaya inachukuliwa kuwa sahihi kwa mujibu wa wanachuoni wengi.

**2.1.3. Nzuri (*hasan* – الحسن )** – hii ni hadithi ambamo kuna japo mtu mmoja katika nyororo ya wapokezi ambaye hajulikani kama ni mkweli na kwamba anasifiwa tu na waandishi wa wasifu wa wapokezi (wataalamu wa *Ilm rijaal*). Aina hii ya hadithi inachukuliwa wanachuoni walio wengi kuwa ni sahihi.

[17] Uchunguzi huu unajulikana kama *'Ilm al-Rijaal* ( علم الرجال ) – wasifu wa wasimuliaji wa hadith

**2.1.4. Dhaifu (*dha'iif* – الضعيف) –** hii ni riwaya ambamo angalau mmoja wa wasimulizi katika sanadi hiyo ni mbaya (mfano ni muongo) au hajulikani. Kwa mujibu wa wanachuoni wengi riwaya dhaifu inaweza ikategemewa madhali tu mafaqihi wa vizazi vilivyopita wametenda kwa mujibu wa riwaya hiyo.[18]

Hadithi *mursnal* zinaweza kugawanyika zaidi kwenye:

**2.2.1 Riwaya *mursal* ya mtu anayetegemewa (*Mursal-u al-thiqah* – مرسل الثقة)** – hii ni riwaya iliyosimuliwa na mtu anayetegemewa lakini ina mwanya kwenye sanad. Au kwa ufasaha zaidi huyo msimuliaji aliyeipitisha hiyo riwaya anajulikana kwa kuwasilisha riwaya kwa kupokea kutoka kwa watu waaminifu wanaotegemewa tu. Kwa mfano, hadithi mursal za Muhammad ibn Abii Umayr zinasemekana kukubalika na sahihi, kwa vile alijulikana kwa kusimulia hadithi zilizopokelewa kutoka kwa mabingwa wanaotegemewa tu.[19]

**2.2.2 Riwaya mursal ya mtu asiyetegemewa (*mursal-u ghayr al-thiqah* – مرسل غيرالثقة)** – hii ni riwaya iliyosimuliwa na watu wasiotambulika kama ni wakweli. Aina hii ya riwaya inachukuliwa kwamba haikubaliki isipokuwa kama mafaqihi wa zamani wameitumia na kufanyia kazi kwa kulingana nayo.

---

[18] Kwa wanachuoni hawa jambo la kwamba mafaqihi waliotangulia wametenda kwa mujibu wa hadithi dhaifu kunaonyesha kwamba kwa hakika lazima iwe walikuwa na ushahidi wa ziada mikononi mwao wa kuithibitisha hadithi hiyo, ambao haupatikani tena kwa sasa hivi miongoni mwetu.

[19] Kwa maoni yanatofautiana juu ya suala hili tazama: *A . Al-Fadhlii, Introduction to Hadith*i (London: ICAS, 2002), uk. 186-189.



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 27 9/9/2015 12:56:02 PM

**Kanuni ya kawaida:** Hivyo, kanuni ya kawaida katika kuitathmini hadithi ni kuona iwapo kama kuna njia yoyote ya kutegemewa ya kuithibitisha hadithi hiyo. Hili linaweza kufikiwa endapo hadithi hiyo itakuwa imehadithiwa na watu wengi, kizazi baada ya kizazi kiasi kwamba haiachi shaka yoyote kuhusu usahihi wake au kama hadithi imepokewa kwa sanadi ya wapokezi waaminifu au kama hadithi inatiwa nguvu na ushahidi wa nje kama vile kukubaliwa na mafakihi wa hapo nyuma au kwa kuwa ya ajabu katika maudhui yake kwa namna ambayo kwamba mtu aweza akathibitisha kwamba hii inaweza kutamkwa na Mtume au Maimam tu basi.



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 28 9/9/2015 12:56:02 PM

# SOMO LA NNE

## MAANDISHI (MATINI)

Mara tu sanadi ya wapokezi inapokuwa imethibitishwa, halafu tunaangalia yale yaliyomo ndani yake, yaani yale maandishi hasa (***al-matn*** – المتن ) ya ile hotuba iliyotamkwa na msimuliaji wa kwanza kabisa wa hadithi hiyo. Maandishi yenyewe yanakuwa na sehemu mbili: maneno yenyewe na maana. Maneno moja moja yanakuwa na aina tatu za maana.

- Maana ya kimsamiati: Hii inapatikana kutoka kwenye mzizi wa neno

- Maana ya kimofolojia: Hii inapatikana kutokana na muundo wa neno lenyewe.

- Maana ya kisarufi: Hii inapatikana kutokana na kazi na nafasi ya neno hilo kuhusiana na hotuba nzima.

Akielezea mielekeo tofauti juu ya yaliyomo, al-Fadhlii anasema:

- Maana hizi tatu kwa hiyo zinapelekea kwenye umuhimu wa jumla, au maana ya jumla: ambayo inapatikana kutoka kwenye maudhui yote nzima.
- Maana zote hizi zinafafanuliwa kwa kurejea msamiati na kwa kutumia kanuni za lugha kimofolojia, kisarufi na kifasaha.

Kati ya viwili hivi, nyororo na maudhui hakuna kinachoweza kusimamishwa kwenye kiwango cha matumizi kama ushahidi kwa ajili ya maamuzi ya kisheria, au kama mamlaka kwa ajili ya kuhojiana.



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 29 9/9/2015 12:56:02 PM

Isipokuwa kama sanadi ya wasimulizi imenyanyuliwa kwanza kwenye kiwango cha usahihi na maudhui ikawa imenyanyuliwa kwenye kiwango cha kufahamika kwa dhahiri kabisa. - (*al-Fadhlii*, 2002, uk. 90)

Hivyo kabla ya kujaribu kufafanua maana ya maandishi ni lazima kwanza tuthibitishe yale maandishi yenyewe halisi hasa, yaani tuhakikishe kwamba yametolewa na Mwenyezi Mungu (katika suala la aya ya Qur'ani) au kutoka kwa Mtukufu Mtume ama Maimam na kwamba hakuna mabadiliko au makosa katika nakala tuliyonayo mikononi leo hii. Bila shaka, katika suala la Qur'ani uhakikishaji wa jumla wa maandishi yake sio lazima kwa vile tunajua kwa uhakika kwamba Qur'ani ni sahihi. Tunachohitaji tu ni kuhakikisha kwamba nakala ya Qur'ani tuliyonayo haina makosa ya chapa na kwamba tunatumia kisomo kinachotegemewa (*al-qira'ah* – القراءة ) cha Qur'ani. Ingawa tofauti za usomaji mara nyingi hazisababishi tofauti ya maana, lakini kuna masuala mengine ambamo maana ya aya inaweza kutofautiana kutokana na usomaji. Kwa mfano, itazame aya ifuatayo:

وَيَسْـَٔلُونَكَ عَنِ ٱلْمَحِيضِ ۖ قُلْ هُوَ أَذًى فَٱعْتَزِلُوا۟ ٱلنِّسَآءَ فِى ٱلْمَحِيضِ ۖ وَلَا تَقْرَبُوهُنَّ حَتَّىٰ يَطْهُرْنَ

**"Wanakuuliza kuhusu hedhi. Waambie: Ni udhia. Basi jitengeni na wanawake wakati wa hedhi, wala msiwakurubie mpaka watwahirike….." (2:222)**

Kama katika aya hiyo hapo juu, neno "يَطْهُرْنَ" litasomeka kama *yatwhurna* basi aya itakuwa inaashiria kukatazwa kujamiiana mpaka mke wake mtu atakapokuwa tohara (yaani kwisha kwa hedhi); lakini kama itasomeka *yatwaharna* basi aya inaashiria kukatazwa



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 30 9/9/2015 12:56:03 PM

kujamiiana mpaka pale mke atakapojitwaharisha (yaani baada ya *al-ghusl* – josho la wajib likisha kuogwa). Hivyo inaweza kuonekana kwamba kwa kubadilika usomaji wa neno moja tu katika aya hiyo kunaweza kusababisha maana tofauti kabisa na kwa hiyo kusababisha hukumu tofauti.

**Uchunguzi wa maandishi (*matn*) ya hadithi:** Kuhusiana na hadithi, baada ya silsila kuthibitika, tunahitaji kuhakikisha maandiko kwa kutafuta kwanza tafsir zote zinazowezekana za kwenye hadithi inayohusika na kuzilinganisha na pili kwa kuamua usomaji mzuri wa hadithi hiyo, kama visomo tofauti vinaweza kuleta maana tofauti. Kwa mfano, kuna hadithi kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ambayo ina neno linaloweza kusomeka kwa namna ya njia mbalimbali:

- *Jaddada*: Hadithi ina maana ya kwamba yeyote atakayetengeneza upya kaburi atakuwa ametoka nje ya Uislam.
- *Haddada*: Hadithi ina maana kwamba yeyote atakayenyanyua tuta kwenye kaburi atakuwa ametoka nje ya Uislam.
- *Jaddatha*: Hadithi ina maana kwamba yeyote atakayemzika mtu mwingine tena ndani ya kaburi ametoka nje ya Uislam.
- *Khaddada*: Hadithi inamaanisha kwamba yeyote anayechimba kaburi (na kuudhihirisha ule mwili wa marehemu wazi) atakuwa ametoka nje ya Uislam.[20]

Kutegemea juu ya ni kisomo gani kilichochukuliwa tunafikia kwenye maana tofauti za hadithi hii. Kwa hiyo mafaqihi hawana budi kuamua ni kisomo gani kati ya visomo hivyo hapo juu ni sahihi kwa ithibati ya riwaya nyinginezo.

[20] *Wasaa'il al-Shi'ah*, Jz. 3, uk. 562 (*Aal al-Bayt*, Jz. 5, uk. 306)



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 31 9/9/2015 12:56:03 PM

Mara itakapokuwa imethibitika kwamba maandishi hayo ni sahihi na tafsiri halisi ikathibitishwa, basi hatua inayofuatia ni kufafanua maana ya maandishi hayo. Katika hatua hii kuna uwezekano namna tatu:

1. **Nass (النص):** Maana ya aina hii zina uwezekano mmoja tu. Maana yake iko wazi na hakuna shaka juu ya kwamba ina maana gani (kauli ya kisheria ya maandishi ya wazi).

**Mfano kutoka kwenye Qur'ani:** Tunasoma kutoka ndani ya Qur'ani:

وَٱلَّذِينَ يَرۡمُونَ ٱلۡمُحۡصَنَٰتِ ثُمَّ لَمۡ يَأۡتُواْ بِأَرۡبَعَةِ شُهَدَآءَ فَٱجۡلِدُوهُمۡ ثَمَٰنِينَ جَلۡدَةٗ وَلَا تَقۡبَلُواْ لَهُمۡ شَهَٰدَةً أَبَدٗا

**"Na wale ambao wanawasingizia wanawake wanaoheshimika kisha wasilete mashahidi wanne, basi watandikeni viboko thamanini. Na msiwakubalie ushahidi wao abadan ….." (24:4).**

Katika aya hiyo hapo juu, neno **abadan -** أَبَدًا linaifanya aya hiyo kuwa wazi zaidi; yaani msikubali ushahidi kutoka kwao kamwe, sio tu kwa ajili ya lile suala lililoko wakati huo.

**Mfano kutoka kwenye hadithi:** Tunapata katika riwaya kwamba, "Kama mtu ambaye yuko katika hali ya Ihram ya Hijja akifunga ndoa huku akijua kwamba imeharamishwa, basi huyo mwanamke anayemuoa anakuwa ni *haram* kwake milele."[21] Tena neno hilo hilo أَبَدًا limetumika katika kuweka wazi kwamba sio kwa kipindi cha wakati ule tu.

[21] *Wasaa'il al-Shi'ah*, Jz. 14, uk. 378 (*Aal al-Bayt*, Jz. 20, uk. 491)



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 32 9/9/2015 12:56:03 PM

2. **Dhaahir ( الظاهر ) –** maana ya aina hii ya maandiko inabeba uwezekano wa namna mbalimbali lakini miongoni mwao kuna moja ambayo inasimama juu ya zote zilizobakia na ambayo iko wazi zaidi katika maana. Ni maana hii ndio inayochukuliwa isipokuwa kama kuna ushahidi wa kuonyesha vinginevyo. Kwa mfano, katika kifungu cha maneno: "Yeye ni ndugu yangu" – neno "ndugu" linaweza kuwa na maana mbili: ndugu halisi wa damu wa baba mmoja, au ndugu katika imani au ndugu katika Uislam. Kutokana na maana mbili hizo hapo juu, ya dhahiri zaidi ni ile ya kwanza.

Imekuwa ni mwenendo wa watu wenye hekima – Waislam na wasiokuwa Waislam – kuchukua ile maana ya dhahiri na wazi zaidi, isipokuwa kama kuna ushahidi wa kuweza kuonyesha vinginevyo. Huu ulikuwa ndio utaratibu pia hata katika wakati wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na Maimam (a.s.) na kwa sababu wao hawakuwahi kuukanusha kamwe, inaonyesha kwamba mwelekeo huu unakubaliwa katika Uislam. Kwa hiyo, mara tu pale maana ya dhahiri inapokuwa imefafanuliwa basi inaweza kutumika.

3. **Mujmal (المجمل) –** maana ya aina hii ya maandiko ni yenye utata kwa vile maandiko hayo yanabeba uwezekano zaidi ya mmoja, hakuna mmojawapo unaomzidi mwenzie. Hivyo faqihi hawezi kuamua lolote kutoka kwenye aina hii ya maandiko.

Kutokana na namna tatu hizo hapo juu za uwezekano wa maana ya maandiko, kundi la kwanza (*Nass*) na la pili (*Dhaahir*) haya yote yanaongozea kwenye upambanuzi wa maana ya maandiko. Kwa hiyo maandiko yanaweza kupambanuliwa katika makundi makuu mawili:

- **Mubayyan (المبين) –** maana ya maandiko iko wazi (inayotokana na *nass* na *dhaahir*)
- **Mujmal (المجمل)** – maana ya maandiko haiko wazi moja kwa moja.

Katika maelezo yanayofuata tutajaribu kuthibitisha maana za wazi (dhaahir) za baadhi ya vifungu vya maneno na miundo ya Kiarabu, kama vile amri na katazo. Baada ya kuthibitisha maana zao za dhahiri, faqihi anaweza akafikia hukumu ya Kiislam inayostahiki kutoka kwenye maandiko yanayozibeba ndani yake.



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 34 9/9/2015 12:56:03 PM

# SOMO LA TANO

## MAAMRISHO NA MAKATAZO

**Amri (*amr* – امر):** Kumekuwa na mijadala mingi kuhusu maana hasa ya amri katika Kiarabu.[22] Baadhi ya wanachuoni wanaielezea amri kama jambo ambalo linasemwa na mtu ambaye ana ubora au mamlaka kumwambia mtu wa hali ya chini, kwa mfano, mwajiri kumwambia mfanyakazi wake. Lakini wanachuoni wengi hawakubali hilo, wakitoa mfano wa ombi mtoto akimwamrisha mzazi wake – hii sio amri ya mkubwa kwenda kwa mdogo. Kwa upande mwingine, inawezekana kuwa na ombi la kawaida tu kutoka kwa mkubwa kwenda kwa mdogo, lisilokusudiwa kuwa amri. Kwa hiyo wanachuoni hawa wanashikilia wazo la kwamba sio lazima kuwa mkubwa bali kuchukulia ukubwa katika wakati wa kuamuru, kama katika suala la mtoto na mzazi wake; na vilevile kwamba sio kila dai kutoka kwa mkubwa kwenda kwa mdogo ni amri, linaweza likawa ni ombi kama kwenye suala la mwajiri kuomba kitu/jambo kutoka kwa mfanyakazi wake.

Kuna njia mbili katika Kiarabu za kumuamrisha mtu kufanya jambo:

- Kutumia kinyambuo kutoka kwenye mzizi "*amr*" (امر) – kinachorejelewa kama *maaddat al-amr* (مادة الامر)
- Kutumia muundo wa amri – unaorejelewa kama *as-Siighat al-amr* ( صيغة الامر )

[22] Mzizi wa neno "amr" رما) ( katika Kiarabu lina maana mbili:
- kitu, mada, jambo. Wingi wa hili ni Umuur (روما)
- amri: Wingi wa hili ni Awaamir (رماوا). Maana tunayoijadili hapa ni hii ya pili – amri.

Mzizi (*maadat al-amr*) – ile maana iliyopendekezwa ya dhahiri ya mzizi wa neno amri ni wajibu. Maana iliyo nyuma ya kauli hii ni kwamba endapo mtu mkubwa akimuomba mtu mdogo kufanya jambo fulani, anawajibika kulifanya isipokuwa labda kuwe na ushahidi mwingine unaoonyesha kwamba haikuwa ni wajibu bali ni pendekezo.

**Muundo** – (*Siighat al-amr*) – maana ya neno kwa neno ya "*siighah*" ni chombo kinachotumika kwa kuundia lakini katika muktadha huu limetumika kurejelea kwenye maumbile tofauti za kuelezea amri bila ya kutumia lile neno hasa la mzizi – *amr*. Baadhi ya mifano ni:

1. Kutumia kitenzi katika sentensi katika wakati uliopo (present tense) ikitanguliwa na herufi Laam **(ل).**
2. Kutumia kitenzi ndani katika sentensi kwenye wakati uliopo tu.

Tena kwa sababu hiyohiyo kama ilivyoelezwa hapo juu, maana ya dhahiri ya amri ni wajibu, isipokuwa labda pawe na ushahidi mwingine unaoonyesha kinyume cha hayo. Kwa ushahidi mwingine tunamaanisha kwamba hakuna aya nyingine au hadithi ambayo inakwenda kinyume na wajibu huo.

Kwa kuhitimisha, hizo hatua tofauti zinazoongozea kwenye kukubalika kwa amri kama ni wajibu, na hivyo kuitumia katika kutoa fatwa (الفتوى) ni:

- Lazima pawe na amri kutoka kwa mkubwa kwenda kwa mdogo
- Kuhakikisha kwamba hakuna ushahidi unaokwenda kinyume



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 36 9/9/2015 12:56:03 PM

**Mfano kutoka kwenye Qur'ani:** Tunasoma ndani ya Qur'ani "Simamisheni Swala!" **(اقيموا الصلاة).** Hiki ni kitenzi cha amri na kwa vile hakuna ushahidi mwingine wa kinyume basi maana ile ya dhahiri inakuwa wajibu. Kwa hiyo aya hii inarejea kwenye wajibu na inaweza kutumika katika kutoa fatwa.

**Mfano kutoka kwenye hadithi:** Ndani ya *Wasail al-Shi'ah* kuna riwaya: "Osheni nguo zenu wakati zinapogusana na mkojo wa mnyama ambaye nyama yake hairuhusiwi kuliwa." Neno lililotumika katika riwaya hii ni "Osha" **(*Ighsil* – اغسل )** ambalo ni neno la amri lenye maana ya dhahiri ya wajibu. Kwa vile hakuna ushahidi mwingine wa kupingana na amri hiyo, basi amri hiyo ni wajibu.

**Neno la amri likitumika katika namna isiyo amri:**

Neno la amri linaweza kutumika katika maana nyinginezo, kama vile:

1. **Sunnah iliyopendekezwa (*Istihbaab* – استحباب):** Kwa mfano, inaweza ikasemwa: "Chukua josho (*ighsil* – اغسل) mnamo siku ya Ijumaa." Neno *ighsil* ni neno la amri kama lilivyoonyeshwa katika mfano wa hapo juu, lakini kwa sababu kuna riwaya zingine ambazo zinatoa ushahidi unaoingilia kati, neno la amri katika hali hii linachukuliwa kama Sunnah iliyopendekezwa.[23]

2. **Ruksa (jawaaz – الجواز):** Hili ni wakati ambapo imefikiriwa kwamba jambo fulani limeharamishwa au liliharamishwa siku za nyuma huko. Kwa hiyo hii ni kutufanya sisi tujue

[23] Mfano mwingine ni "Osha uso wako – mara moja kama wajibu na mara ya pili kama isbaagh ( اسباغا )**"** Neno hilohilo "ighsil" limetumika mara zote, lakini tunajua kwamba ni ile Osha ya kwanza tu ndio ambayo ni ya wajibu na huku kuosha kwa mara ya pili, ni sunnah iliyopendekezwa.



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 37 9/9/2015 12:56:03 PM

kwamba katazo hilo limeondolewa. Kwa mfano, tunasoma ndani ya Qur'ani: وَإِذَا حَلَلْتُمْ فاصطَادوا **.... Na mkishatoka kwenye Hijja, basi windeni ..... (5:2).** Ingawa hapa "windeni" iko katika hali ya amri, inachukuliwa kumaanisha ruksa kwa sababu ndani ya wakati wa Ihraam kuwinda kumeharamishwa na kukatazwa huku kunaondoka baada ya kuvua Ihraam.

# MAKATAZO

**Makatazo (nahy – النهى):** Hili ni kinyume na Amr – kwani ni mtu mkubwa anamtaka mtu mdogo asifanye jambo fulani, yaani kumzuia asifanye tendo fulani.

Kama hapo kabla, hoja inaibuka – kama iwe ni mtu ambaye ni mkubwa au mtu tu ambaye anajipatia umaarufu na iwapo kama ikisemwa na mtu mkubwa je ni lazima iwe inachukuliwa kama katazo au inaweza ikawa kama ni ombi la kawaida tu. Kwa mara nyingine tena majibu yaliyotajwa hapo juu yanaweza kutolewa.

Kuna njia mbili katika Kiarabu za kumkataza mtu kufanya jambo:

- Kutumia umbo la kinyambuo cha mzizi "*nahy*" (ن ه ي – lililorejelewa kama *maaddat al-Nahy* (مادة النهي).
- Kutumia umbo la katazo – lililorejewa kama *Siighat al-nahy* (صيغة النهي)

**Mzizi (*maaddat al-nahy*) –** maana ya dhahiri iliyopendekezwa ya mzizi *"nahy"* ni katazo. Kwa hiyo, kama ikitamkwa na mtu mkubwa kumwambia mtu mdogo na hakuna ushahidi mwingine ambao unaweza kwenda kinyume na maana hii ya dhahiri basi

inachukuliwa kama ni katazo. Kwa mfano, tunasoma ndani ya Qur'ani Tukufu:

إِنَّ ٱللَّهَ يَأْمُرُ بِٱلْعَدْلِ وَٱلْإِحْسَٰنِ وَإِيتَآيِٕ ذِى ٱلْقُرْبَىٰ وَيَنْهَىٰ عَنِ ٱلْفَحْشَآءِ وَٱلْمُنكَرِ وَٱلْبَغْىِ

**"Hakika Mwenyezi Mungu anaamrisha uadilifu na hisani na kuwapa jamaa na anakataza uchafu na uovu na dhulma….." (16:90)**

**Muundo (*Sighat al-Nahy*)** – Hapa tena kuna njia tofauti za kuelezea hiyo amri bila ya kutumia ule mzizi wenyewe hasa "nahy." Baadhi ya mifano ni:

1. Kutumia kitenzi cha katazo katika sentensi, yaani kutumia 'Laa' ya katazo ikifuatiwa na wakati uliopo (*present tense*) wa hicho kitenzi bila ya irabu juu ya herufi ya mwisho ya kitenzi, mfano – Laa tadhlim – لاتظلم – **'Usidhulumu!"**
2. Kutumia mfano wa tahadhari, *tahdhiir* (**التحذير**) kwa mfano, *Iyaka an takdhib* (إياك ان تكذب) Jihadhari na kudanganya!"
3. Kutumia maelezo au kauli (*al-Jumlat al-khabariiy* - الجملة الخبرية ) kwa mfano baba anaweza kumwambia mwanawe, "Wewe usicheze na kibiriti!" akiwa na maana kwamba usicheze na njiti za kiberiti. Kauli hii lazima ichukuliwe kama katazo ingawa imeundwa katika namna ya maelezo.

Akili zetu zinatueleza kwamba wakati wowote tunapokuwa na aya au hadithi ambayo maana yake ya dhahiri ni katazo ni lazima tuitii hiyo isipokuwa kama kutakuwa na ushahidi wa kinyume chake. Kwa hiyo kama kuna amri/katazo kutoka kwa mkubwa bila ya ushahidi



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 39 9/9/2015 12:56:04 PM

pinzani, basi hiyo *Amr/Nahy* itakuwa ni uthibitisho (*hujjah* – الحجَة) na inaweza kutumika katika kutolea hukumu za kisheria.

**Mfano kutoka kwenye Qur'ani:** Tunasoma kutoka ndani ya Qur'ani:

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لَا تَأۡكُلُواْ ٱلرِّبَوٰٓاْ

**"Enyi ambao mmeamini msile riba ….." (3:130)**

Hili ni katazo kutoka kwa Aliyejuu juu Mkubwa – Mwenyezi Mungu na hakuna ushahidi mwingine ndani ya Qur'ani au Sunnah inayoruhusu riba, kwa hiyo hakuna ushahidi unaopingana na hivyo aya hii inakuwa uthibitisho (*hujjah*) wa uharamu/katazo hilo.

**Mfano kutoka kwenye hadithi:** Ndani ya *Wasa'il al-Shi'ah* kuna riwaya: "Usimuoe binti ya kaka au dada yake mkeo bila ya idhini ya mkeo." Maana ya dhahiri ya hadithi hii ni ule uharamu wa ndoa hiyo (bila idhini ya mke) na hakuna ushahidi unaopingana nayo. Kwa hiyo tunaweza kuamua kwamba ni haram mtu kumuoa mtoto wa dada au wa kaka wa mke wake bila ya ridhaa ya mke wake.

**Neno la makatazo kutumika katika muundo wa kutokatazwa:** Neno la mkatazo linaweza kutumiwa kwa maana nyinginezo kama vile machukizo. Kwa mfano, tunakuta kwamba katika baadhi ya riwaya tunaambiwa tusichukue udhu kwa maji yaliyopashwa moto na jua la moja kwa moja na pia usitengeneze kinyunya na maji kama hayo ya joto la jua kwani yanasababisha mbalanga (*al-baras* – البرص ). Hadithi hii inaashiria kwamba matendo haya yana machukizo na kwamba ni bora kuepuka kuyatenda, kwa sababu mwishilizio wake unapelekea kuhitaji ushauri wa daktari, ikimaanisha kwamba ni bora kuchukua tahadhari. Kwa hiyo huu ni ushauri na sio makatazo.



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 40 9/9/2015 12:56:04 PM

# SOMO LA SITA

## MAANA YENYE KUJITOKEZA

Maana yenye kujitokeza (*al-Mafhuum* – المفهوم ni ile maana inayotumika ya neno au sentensi au kifungu cha maneno ambayo inaeleweka kutokana na maandishi kwa njia ya matumizi. Hii ni kinyume na ile maana ya kuzungumzwa (*al-mantuuq* – المنطوق) ambayo inaelezewa kwa dhahiri. Kwa mfano, tunasoma ndani ya Qur'ani:

فَلَا تَقُل لَّهُمَآ أُفٍّ

**"…basi usiwaambie (wazazi wako) Ah!.." (17:23)**

Maana ya dhahiri ya kauli hiyo ni kwamba mmekatazwa kuwaambia wazazi wenu Ah! Hata hivyo, maana ya kauli hii ambayo inajitokeza ni kwamba umekatazwa kuwafanyia wazazi wako madhara ya aina yoyote (ya kiakili na ya kimwili). Au tunasoma katika hadithi, "Kama ukilala udhu wako unakuwa batili." Maana ya dhahiri ya maneno haya ni kwamba udhu unatenguliwa na usingizi. Maana inayojitokeza kwenye kauli hii ni kwamba kama hukulala basi udhu wako bado ni halali (madhali hakuna kati ya mengine yanayotengua udhu lililotokea) – kwa hiyo hakuna kipengele cha mipaka ya muda wa uhalali wa udhu.

**Maana iliyodokezwa imegawanyika mara mbili:**

1. **Inayoafikiana na maana inayojitokeza (*mafhuum al-muwaafaqah* – مفهوم الموفقة)** ni pale maana inayojitokeza



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 41 9/9/2015 12:56:04 PM

na ile maana ya dhahiri zinapokuja kukubaliana na kupatana pamoja. Kama tulivyoona katika mfano hapo juu wa mtu kumwambia mzazi wake "Ah" maana zote mbili, ya kujitokeza na ya dhahiri ni za namna moja – ya makatazo. Mfano mwingine unaweza kupatikana katika riwaya ndani ya *Wasa'il Shi'ah* ambayo inaeleza kwamba endapo jasho la ngamia ambaye amekula kinyesi cha mwanadamu (*jallaala* - الجلالة ) likaja likakutana na ngozi yako basi uioshe. Maana inayojitokeza katika riwaya hii ni kwamba jasho la ngamia kama huyo ni najisi na kwa hiyo tunaambiwa tuoshe ngozi iliyogusana nayo.

2. **Mafhuum al-mukhaalafah (مفهوم المخالفة)** ni wakati hukumu iliyotajwa kwa kudokeza na hukumu iliyotajwa kwa dhahiri zinapokuwa sio za namna moja, yaani zote sio za amri wala sio zote za makatazo. Hapa zile maana za kudokeza na za dhahiri zinagongana na ziko kinyume na kila mojawapo. Katika mfano wa hapo juu wa udhu kubatilishwa na kulala – kama utasinzia, udhu utakuwa batili, lakini kama hukulala na kusinzia udhu wako unabakia kuwa halali – zote ziko kinyume na kila mojawapo. Mfano mwingine ni ile riwaya inayoeleza kwamba kama kondoo hakuchinjwa sawasawa (kwa mujibu wa sheria ya Kiislam) hawezi kuliwa. Maana inayojitokeza katika hadithi hii ni kwamba kama kondoo huyo akichinjwa sawasawa basi anaweza kuliwa – mmoja anakatazwa na mwingine anaruhusiwa – wote wana tofauti kati ya mmoja na mwingine.

**Mafhuum al-mukhaalafah imegawanyika mara sita:**

a. Maana yenye masharti au maana ya wazi ya sentensi yenye masharti (*mafhuum al-shart* – مفهوم الشرط )

b. Maana Inayoambatana na Sifa au maana ya wazi ya kivumishi (*mafhuum al-wasf* – (مفهوم الوصف)

c. Maana yenye ukomo (wa wakati) au maana ya wazi ya mwisho (*mafhuum al-ghaaya* – مفهوم الغاية)

d. Maana iliyofungika au maana hasa ya mfungiko/mabano (mafhuum al-hasr – مفهوم الحصر )

e. Maana ya kiidadi au maana hasa inayoegemea kwenye kiwango (*mafhuum al-'adad* – مفهوم العدد)

f. Maana ya kisifa cha jina au jina la kisifa - lakabu (*Mafhuum al-laqab* – مفهوم اللقب).

Katika kinachofuatia sisi tumeyazungumzia hayo matatu ya mwanzoni tu.

## MAANA YENYE MASHARTI

Kuwa na maana yenye masharti ni lazima kuwe na sharti ndani ya sentensi hiyo. Kwa mfano katika sentensi: "Kama ukimuona mwanachuoni ni lazima umheshimu." Hiyo heshima ni kwa sharti la kumuona mwanachuoni.[24] Maana ya dhahiri ya aina hii ya kauli ni kwamba, kama sharti halikuthibitishwa basi hakuna wajibu – ikiwa na maana kwamba huna haja ya kwenda huku na huko kutafuta mwanachuoni wa kumpa heshima. Mfano mwingine: "Kama ukizungumza wakati wa swala, basi swala hiyo ni batili." Sharti la kubatilika kwa swala ni kuzungumza ndani yake. Maana ya dhahiri ya kauli hii ni kwamba kama hutazungumza wakati wa swala, ama ukazungumza nje yake, basi swala ni thabiti.

[24] Kama sentensi ingekuwa "Heshimu Mwanachuoni." Kusingekuwa na sharti.

Kwa hiyo, wakati wowote sharti linapoondolewa, hukumu pia inaondolewa. Hata hivyo kuna masharti manne kwa hitimisho hili.

**1.** Lazima kuwe na uhusiano namna mbili kati ya sharti na hukumu, sio sadifa tu peke yake (*al-ittifaaq*).

**2.** Hiyo sentensi yenye masharti lazima iwe na maana kwamba kile kifungu chenye masharti kinafuata lile sharti linalowasilishwa.

**3.** Sharti la tatu na la muhimu sana ni kwamba ni lazima tuhakikishe kwamba sharti hili la kipekee maalum ni kwa ajili ya hicho kifungu chenye masharti, kwa mfano: "Kama jiko linafanya kazi, basi kutakuwa na joto." Hapa dhana ya wazi inaweza kuhitimishwa ni kwamba kama jiko halifanyi kazi, kutakuwa na baridi – hata hivyo, hii sio lazima iwe ni kweli kwa sababu jua linaweza kuwa linawaka. Hapa sharti sio la kipekee kwa ajili ya kile kifungu chenye masharti.

**4.** Ni lazima kuwe hakuna ushahidi unaopingana.

Kama masharti yote manne yakipatikana, basi maana dhahiri yenye masharti inaweza kuthibitibika. Mfano wa Qur'ani ni aya ya: **"Basi atakayekuwa mjini katika mwezi huu naaufunge;…." (2:185)** – sharti hapo ni kwamba, mwezi wa Ramadhani lazima uwepo kwa ajili ya wajibu wa kufunga. Maana ya dhahiri ya sentensi hii ni kwamba yeyote ambaye hatakuwepo katika mwezi wa Ramadhani hatakiwi kufunga.

Mfano kutoka kwenye hadithi ni kwamba Imam as-Sadiq (a.s.) aliulizwa kuhusu kondoo aliyekuwa anachinjwa, ambaye hakuonyesha mtikisiko au athari wakati wa kufa kwake, ingawa damu alimwagika kama kawaida. Imam (a.s.) alijibu akasema: "Msile kondoo huyo," na

akaongeza kusema, "Imam Ali (a.s.) amesema kwamba kama miguu ikisogea na macho yakipepesa wakati wa kuchinjwa basi mnaweza mkala." Kutokana na hayo hapo juu tunaweza kuona kwamba Imam as-Sadiq (a.s.) alihoji kupitia maana ya wazi kwa kutumia sentensi yenye masharti ya Imam Ali (a.s.).

## MAANA INAYOAMBATANA NA SIFA

Katika Kiarabu, neno "*wasf*" lina maana ya sifa au tabia. Katika sarufi ya Kiarabu, *wasf* maana yake ni kivumishi, yaani neno ambalo linaelezea nomino iliyotangulia. Hili neno linaloelezea linaitwa wasif na lile "*wasf*" au "*sifah*" na lile neno linaloelezewa linaitwa "*mawsuuf*" - (الموصوف). Swali hapa katika *Usuul al-fiqh* ni, "wakati sifa ikiondolewa kutoka kwenye jambo, je tunaweza kuhoji kwamba na hukumu imeondolewa vilevile? Kwa mfano, katika hukumu "Heshimu watu wenye elimu," kama sifa ya elimu ikikoma kuwepo, je hiyo hukumu ya heshima bado itaendelea kuwepo? Kwa maneno mengine, hukumu hiyo bado inatumika baada ya sifa kuondolewa? Wale wanaoamini maana iliyoambatana na sifa wanashikilia kwamba mara tu ile sifa inapoondolewa na hukumu nayo pia huondolewa.

Kuna masharti mawili kwa ajili ya maana ya inayoambatana na sifa:

i. Sifa hiyo lazima iwe ni sharti kwa ajili ya kufanyia hukumu

ii. Ni lazima pawe hakuna ushahidi mwingine wa kinyume.

Mfano wa kutoka kwenye Qur'ani ni:

حُرِّمَتۡ عَلَيۡكُمۡ أُمَّهَٰتُكُمۡ وَبَنَاتُكُمۡ وَأَخَوَٰتُكُمۡ وَعَمَّٰتُكُمۡ وَخَٰلَٰتُكُمۡ وَبَنَاتُ ٱلۡأَخِ
وَبَنَاتُ ٱلۡأُخۡتِ وَأُمَّهَٰتُكُمُ ٱلَّٰتِيٓ أَرۡضَعۡنَكُمۡ وَأَخَوَٰتُكُم مِّنَ ٱلرَّضَٰعَةِ وَأُمَّهَٰتُ
نِسَآئِكُمۡ وَرَبَٰٓئِبُكُمُ ٱلَّٰتِي فِي حُجُورِكُم مِّن نِّسَآئِكُمُ ٱلَّٰتِي دَخَلۡتُم بِهِنَّ فَإِن لَّمۡ تَكُونُواْ
دَخَلۡتُم بِهِنَّ فَلَا جُنَاحَ عَلَيۡكُمۡ وَحَلَٰٓئِلُ أَبۡنَآئِكُمُ ٱلَّذِينَ مِنۡ أَصۡلَٰبِكُمۡ وَأَن
تَجۡمَعُواْ بَيۡنَ ٱلۡأُخۡتَيۡنِ إِلَّا مَا قَدۡ سَلَفَۗ إِنَّ ٱللَّهَ كَانَ غَفُورٗا رَّحِيمٗا ﴿٢٣﴾

**"Mmeharamishiwa mama zenu, na binti zenu, na dada zenu na shangazi zenu na khalat zenu, na binti wa kaka na binti wa dada, na mama zenu waliowanyonyesha na dada zenu wa kunyoyonya, na mama wa wake zenu na binti zenu wa kambo walio katika ulinzi wenu, waliozaliwa na wake zenu mliowaingilia-hapana vibaya juu yenu ikiwa hamkuwaingilia-na wake wa watoto wenu waliotoka katika migongo yenu, na kukusanya kati ya dada wawili, ila waliokwisha pita. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu" (4:23).**

Katika aya hii, ndoa na binti wa kambo aliyezaliwa na mke ambaye mtu amekamilisha naye ndoa kwa vitendo imekatazwa, ni haramu. Kama sifa hii haitakuwepo basi na hukumu itabatilika.

Mfano kutoka kwenye hadithi, *Wasa'il al-Shi'ah*: "Yule ambaye ana mali (tajiri) na akafanya isivyostahili katika mkopo atakuwa anafanya dhulma."

Sifa zilizoainishwa hapa kwa mtu anayefanya makosa katika mkopo ni:

1. Kuwa tajiri
2. kutokulipa deni



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 46 9/9/2015 12:56:05 PM

Kwa hiyo katika suala hili, sifa zote mbila ni lazima zipatikane ili hukumu hiyo iwe ya sahihi.

Ile hukumu "Heshimu Mwanachuoni" haiwezi kuainishwa kama dhana vumishi kwa sababu sifa yake haikutanguliwa na nomino kama katika mfano wa "Mheshimu mtu ambaye ni mwanachuoni" ambao unaweza kuchukuliwa kama dhana vumishi.

- **Maana yenye ukomo (wa wakati)**

Hili neno 'Ghaayat' lina maana ya "mwisho." Kuamini maana yenye ukomo kuna maana kwamba wakati kukiwa na hukumu ambayo ndani yake mwisho ama kiwango vimeainishwa, kwa kawaida kutumia lile neno "mpaka," na uondoaji wa mwisho au wa mpaka kunasababisha uondoaji wa hukumu. Mfano wa Qur'ani ni aya:

ثُمَّ أَتِمُّواْ ٱلصِّيَامَ إِلَى ٱلَّيۡلِۚ

**"….Kisha timizeni saumu mpaka usiku ….." (2:187)**

Kwa hiyo, baada ya kuzama kwa jua mtu hatakiwi kuendelea kufunga. Mfano kutoka kwenye hadithi ni: "Kila kitu ni halali **mpaka** pale kitakapothibitishwa kuharamishwa kwake." Kwa hiyo kama kitu hakikuthibitishwa kuwa ni haramu basi kitu hicho ni halali na kinaruhusika kutumiwa.

Kuna shuruti mbili kwa ajili ya hiyo maana yenye ukomo:

- Huo mwisho lazima uwe ni sharti la hukumu
- Ni lazima kusiwe na ushahidi mwingine wenye kukinzana

# SOMO LA SABA

# KANUNI ZA JUMLA NA ZA MAALUM

## KANUNI ZA JUMLA DHIDI YA ZILE ZA UMAALUM:

Zile za jumla (*'Aamm* العام )ni aina ya usemi ambao unajumuisha watu wote kwa kutumia mitindo fulani ya kilugha au maneno fulani kama "wote," "kila"[25] na kadhalika. Hata hivyo, hizo maalum (*al-khaass* -الخَاصْ) ni aina ya usemi ambao unajumuisha tu baadhi ya watu. Kwa mfano, ile kanuni ya "Heshimuni wanachuoni wote," ni kanuni ya ujumla kwa sababu neno "wote" haliainishi ni wanachuoni gani na kwa hiyo linajumuisha wanachuoni wote. Aidha, ile kanuni ya: "Heshimuni wanachuoni wote isipokuwa wale wanaopotoka" ni kanuni maalum kwa sababu neno "isipokuwa" linaivumisha kauli hiyo na kuweka mpaka wa amri hiyo kwa wale wanachuoni ambao sio wapotofu wenye kupituka mipaka.

Wakati mwingine huo ujumla unaashiriwa kwa neno kama "wote" na wakati mwingine kwa matumizi ya mtindo maalum. Kwa mfano, kwa Kiarabu wakati nomino isiyo na mpaka wa dhahiri (*nakarah* – نكَرَة ) ikitumika katika sentensi hasi inaonyesha ujumla, kama vile "*Maajaa'a rajulun* – ماجاء رَجل" ambayo maana yake ni "Hakuna mtu aliyekuja." Kadhalika wakati katazo likiwa linahusika kwenye nomino isiyo na kikomo huwa inaashiria kwenye ujumla, kama vile: "Usimuapie au kumzushia mtu yeyote uongo."

[25] Maneno ya Kiarabu ambayo yanaonyesha ujumla ni pamoja na "kull – كُلّ", "jamii' – جَمِيْع" "Aammah – عَامَة" "kaffah – كَافَة," "tamaam – تَمَام" na "ayy – .أَي"

Kwa Kiarabu, kama muundo wa wingi ukitanguliwa na kibainishi kilicho wazi, ambacho ni “al-“ basi inaashiria pia ujumla, kama vile “*Akrim al-‘ulamaa*” ambacho maana yake ni “Waheshimu wanachuoni (wote).” Hili limeafikiwa na wanachuoni wote.

Mfano wa kutoka kwenye Qur’ani ni ile aya ya 222 ya Sura ya 2:

إِنَّ ٱللَّهَ يُحِبُّ ٱلتَّوَّٰبِينَ

**“Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wenye kutubia” (2:222).**

Baadhi ya wanachuoni wanaamini kwamba hata kama nomino moja imetanguliwa na kibainishi kilicho wazi kama “*Akrim al-Aalim*” basi inaonyesha ujumla, lakini hili ni wazo ambao halishikiliwi na wengi wa wanachuoni.

## AINA TOFAUTI ZA UJUMLA:

Kuna aina tatu za ujumla kama ifuatavyo:

1. **Al-‘umuum al-istighraaqii ( العمُوم الاستِغراقِي ) – Yote au kila kitu:**

Hii ni aina ya ujumla ambayo inajumuisha wote wanaowezekana kuhusika na istilahi ya jumla. Kwa mfano, wakati inaposemwa: “ احترم كل عالِم ” “Heshimu wanachuoni wote” amri hiyo inajumuisha wanachuoni mmoja mmoja wote kwa jumla. Kama mathalan kuna wanachuoni 100, basi tunapaswa kuwaheshimu wote. Kama tukionyesha heshima kwa 99 tu kati  yao, basi tutakuwa tumekamilisha asilimia 99% tu ya hukumu hiyo na tutahukumiwa ipasavyo. Kwa maneno mengine ni kwamba tumetii kuhusiana na

watu 99 na tumekaidi kuhusu kumtii mmoja. Kwa hakika, katika aina hii ya maelezo hukumu inazidishwa kulingana na kila suala na mmoja wao anamaanishwa na kuhusishwa kipekee.

**2. Al-umuum al-majmuu'ii ( العموم المجموعي ) – wote:**

Hii ni aina ya ujumla hali ya kuwa moja moja inachukuliwa kwa pamoja au kwa mkusanyiko na kwa hiyo utii au ukaidi kuhusiana na hukumu hiyo unategemea juu ya hali yote ndani ya kundi lililowekwa. Kwa mfano, pale inaposemwa: "Fungeni kuanzia kuchomoza kwa jua hadi kuzama kwa jua," muda wote kati ya mawio na machweo unamaanishwa kama ni kitu kizima kimoja, sio kila saa moja kipekee. Kwa hiyo, iwapo mtu atafunga kwa 99% tu ya kipindi cha muda kati ya mawio na machweo, basi saumu hiyo itakuwa ni batili na yeye hatapata malipo yoyote kwa ajili yake hiyo.

**3. Al-'umuum al-badalii ( العموم البدلي ):**

Kwa Kiarabu, neno "badal" lina maana ya "mbadala." Katika aina hii ya ujumla hakuna mmoja maalum anayemaanishwa na ni mmoja wao tu anayehitajika. Kwa mfano, pale inaposemwa: "Mwachie mtumwa yoyote unayemtaka" hapo inatosha kuachia huru mtumwa yoyote.

## AINA TOFAUTI ZA UMAALUM

Kuna aina mbili za umaalum:

**1. Al-khaass al-muttasil ( الخاص المتصل )**

Hii inarejelea kwenye umaalum ambao umetajwa katika kifungu hicho hicho cha maneno ambamo ujumla umetajwa.



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 50 9/9/2015 12:56:06 PM

## 2. Al-khaass al-munfasil ( الخاص المنفصل )

Hii inarejelea kwenye umaalum ambao haukuunganishwa ama ulioachanishwa kutoka kwenye ujumla. Hapa hukumu ya ujumla ilikuwepo na ilitimizwa kikamilifu, lakini tena baadaye ikabadilishwa na ile kanuni ya umaalum.

Katika miundo yote ya umaalumishaji na ujumuishaji, kile kinachoashiria umaalum kinakiweka pembeni kile kinachoashiria ujumla. Hata hivyo, katika umaalum uliounganishwa (*Al-khaass al-muttasil*) ujumla hauchukui sura kabisa. Hii ni kinyume na umaalum ulioachanishwa ambamo ujumla unachukua sura, lakini baadaye unakuwa umeondolewa na kuwekewa ukomo na kile kinachoashiria umaalum.[26] Kwa mfano, aya ya Qur'ani inaweza yenyewe ikawa ya jumla na kisha ikawa ya maalum kutokana na aya nyingine au hadithi. Kwa hiyo, ni muhimu kuzingatia rejea zote za Qur'ani na hadithi zinazohusika kwenye hukumu fulani kabla ya mtu kuweza kuamua iwapo kama hukumu imemaanishwa kuwa ya ujumla au umaalum.[27]

[26] Ni lazima izingatiwe kwamba wakati ujumla unapochukua sura na halafu baadae ikawa umekatazwa, tunaweza kutumia ile kanuni ya jumla kwenye suala ambalo halijulikani kuwa limeondolewa kutoka kwenye jumla ile ya maalum. Kwa mfano, kama ikisemwa, "Heshimu wanachuoni wote!" na halafu baadae ikasemwa: "Usiwaheshimu wanachuoni wasio waadilifu (watenda dhambi)!" na tunadhani kwamba kutokuwa mwadilifu kuna maana ya kutenda madhambi makubwa au kutenda ama dhambi kubwa au ndogo, matokeo yatakuwa kwamba mwanachuoni aliyetenda dhambi ndogo atabakia chini ya kanuni ya jumla na ni lazima aheshimiwe. Hii iko hivyo kwa sababu mwanachuoni kama huyo kwa hakika amejumuishwa katika ile ya jumla na tuna shaka kwamba huenda kwa ile ya maalum ama hapana.

[27] Ni kawaida kabisa miongoni mwa mifumo mbalimbali ya kisheria kwanza kabisa kuwa na kanuni ya kawaida iliyotolewa na chombo cha sharia kama vile bunge na kisha kuwa na maelezo na mabadiliko yaliyofafanuliwa katika hatua ya baadae na chombo hichohicho ama vyombo vingine kama vile serikali. Kwa nyongeza ya jambo hili la kawaida, inapasa kuzingatiwa kwamba Uislamu, kama dini kamili, ulikuja hatua kwa hatua, na Qur'ani ilishushwa kwa kipindi cha muda, kwa hiyo, watu walipewa kwanza maagizo ya jumla na miongozo na kisha, baada ya kuwa wamejiandaa, walipewa hukumu zenye maelezo na maalum. Kabla ya kutumia hukumu ya jumla, tunapaswa kuangalia kwamba hakuna makatazo yaliyofanywa na maelekezo muhimu.



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 51 9/9/2015 12:56:06 PM

# KANUNI ZA UMAALUM NA KIMASHARTI

Maalum (*al-Mutlaq* - المُطلَق) ni neno ambalo linajumuisha watu wote, sio kwa njia ya kisarufi bali kwa utimizaji wa "masharti ya hekima" (*muqaddamaat al-hikma* – مقدمات الحكمة). Hivyo ile ya maalum ni tofauti na ile ya jumla ambayo inaashiria ujumla kilugha. Katika kauli ya maalum au isiyo na masharti, hakuna maneno kama hayo yanayotumika na maelezo yanachukuliwa kuwa ni ya jumla baada ya wazo la kihekima, yaani, kwa sababu hakuna umaalum uliotajwa, ni lazima itamaanisha ujumla. Mfano kutoka kwenye Qur'ani ni aya ya 2:275:

وَأَحَلَّ ٱللَّهُ ٱلْبَيْعَ

**".....Mwenyezi Mungu amehalalisha biashara....." (2:275)**

Aya hiyo hapo juu inaashiria kwamba aina zote za biashara au uchuuzi zinaruhusiwa kwa vile hakuna katazo lililowekwa hapo. Hivyo, kuharamisha biashara au shughuli za uchuuzi kunahitaji sababu ya ziada au ya pili. Mfano mwingine wa Qur'ani ni aya ya 4:92.

Yenye masharti (*al-muqayyad* - المقيد) ni neno ambalo halijumuishi watu wote. Kwa mfano, pale inaposemwa: "Mwache huru mtumwa muumini" hukumu hiyo sio tena isiyo na masharti kwa sababu ya lile sharti la "muumini" kuhusiana na mtumwa huyo.

Kama ilivyokwisha kuelezwa, ujumuishwaji wa ile ya maalum unaamuliwa kwa hoja ya kimantiki. Kwa kusimama ile ya maalum, masharti yafuatayo lazima yatumike:

1. Ingekuwa ni lazima kwa mzungumzaji kuweka katazo au sharti, kama angetaka kufanya hivyo, katika mawasiliano yao. Kama hawakufanya hivyo, ilikuwa ni nje ya hiari yao.

2. Lazima kuwe hakuna ushahidi kwamba mzungumzaji alimaanisha sharti lolote kwa hali yoyote ile iwayo.

3. Mzungumzaji lazima awe na nia ya kutoa maelezo yote ili msikilizaji aweze kufanyia kazi hayo mawasiliano, ili kwamba isiwe imesemekana tu hivi kwa lengo la mjadala au kuandaa hatua nyingine ambamo maelezo yanayotakikana kwa ajili ya utendaji wa sawasawa uweze kutajwa.

Kwa hiyo, ili faqihi aweze kuhitimisha fatwa ya kidini kutoka kwenye aya fulani au hadithi ni lazima kwanza aelewe hayo maudhui na pili atafute kama kuna makatazo yoyote ambayo yanaweza yakabadili maandiko kutoka kwenye umaalum kwenda kwenye ya kimasharti. Pia ni baada ya ukamilishaji wa masharti hayo hapo juu ya hekima ambapo faqih anaweza kuamua kwamba fatwa hiyo inatumika kwa watu wote.

# SOMO LA NANE

## KANUNI ZA KILUGHA

Wakati mtu anaposoma maandiko, inaweza kusiwe na shaka kuhusu maana halisi hasa ya maandiko hayo lakini kunaweza kuwa na shaka kuhusu iwapo kama mwandishi wa maandiko hayo alikusudia hasa ile maana ya neno kwa neno au hapana. Kwa mfano, mtu anaposoma neno "simba" maana yake halisi ni yule mnyama simba, lakini kinachoweza kumaanishwa hapo na mwandishi ni maana ya kiistiari, yaani mtu shujaa. Kanuni za kilugha (*al-usul al-lafdhiyyah* – الاصول اللفظية) zinakuwepo kutuelekeza sisi juu ya jinsi tunavyoweza kueleza ni nini hasa kilichomaanishwa katika mas'ala hayo.

Kanuni za kilugha zilizo muhimu kabisa ni kama zifuatazo:

1. **Uasilia wa maana halisi (***aswaalat al-haqiiqah* – اصالة الحقيقة **):** Wanachuoni wote wanakubaliana kwamba, labda kuwe na ushahidi wa kupendekeza vinginevyo, laa sivyo maana ya kweli na halisi ya maandiko inapaswa kukubalika kwa wote, kwani huu ndio mtazamo wa binadamu mwenye busara.
2. **Uasilia wa ujumla (***aswalaat al-'umuum* – اصالة العموم **):** Kanuni hii inatumika kwenye mas'ala ambamo mtu anakuwa na shaka iwapo ni maana ya jumla au maalum inayokusudiwa humo. Katika hali hii, mtu lazima atwae ujumla labda kama kuna ushahidi wa kuonyesha vinginevyo.
3. **Uasilia Usiofungwa (***aswalaatal-itlaaq* – اصالة الاطلاق**)** Kanuni hii inatumika pale mtu anapokuwa na shaka iwa-

po kama hukumu katika mas'ala hiyo imekusudiwa bila ya masharti au ni wa kimasharti. Kwa hali hii, mtu lazima achukue ile ya kwanza, labda kama kuna ushahidi wa kuonyesha vinginevyo.

**Mazingatio:** Baadhi ya wanachuoni wamependekeza kwamba kanuni zote hizo hapo juu zinaweza kuletwa pamoja chini ya kichwa kimoja ambacho ndio uasili wa muonekano wa dhahiri (*aswaalat al-dhuhuur* – اصالة الظهور). Kulingana na hili, labda iainishwe vinginevyo, lakini maana ya dhahiri ndio ya kuchukua kipaumbele.

# UHUSIANO KATI YA QUR'ANI NA SUNNAH

Uhusiano kati ya fatwa zilizotajwa ndani ya Qur'ani na zile zilizotajwa ndani ya Sunnah (hadithi) zinaweza kuwekwa katika madaraja kama ifuatavyo:

1. **Utungaji Sheria (*al-tashrii* - التشريع)**: Hii ni fatwa ambayo sheria yake imetajwa katika Sunnah na sio katika Qur'ani kama fatwa ya kwamba muuaji harithi kutoka kwa muathirika wake au kwamba mwanaume haruhusiwi kumuoa mtoto wa dada au wa kaka wa mke wake bila ya ruhusa kutoka kwa mke wake.
2. **Msisitizo (*al-ta'kiid* - التأكيد):** Hii ni fatwa ambayo imetungiwa sheria ndani ya Qur'ani na kusisitizwa katika Sunnah, kama vile wajibu wa swala, swaumu, kuamrisha mema na kukataza ulevi wa pombe na mauaji.
3. **Kubainisha (*al-bayaan* - البيان)** Hii ni fatwa ambayo imetungiwa sheria ndani ya Qur'ani na kutafsiriwa au kuelezewa zaidi na Sunnah. Aina hii ya hukumu inaweza kugawa-



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 55 9/9/2015 12:56:06 PM

nywa katika sehemu tatu:

**3.1 Maelezo (*al-tafsil* - التفصيل):** Hii ni fatwa ambayo imetungiwa sheria ndani ya Qur'ani na maelezo zaidi yanatolewa katika Sunnah. Kwa mfano, Qur'ani inasema: "simamisheni swala," lakini mpangilio wa swala umeelezwa bayana katika hadithi.

**3.2 Kuzuilia (*al-takhsiis* - التَخصيص)** Hii ni fatwa ambayo imetungiwa sheria ndani ya Qur'ani kama hukumu ya jumla na ikawekewa mipaka katika Sunnah. Mfano kutoka kwenye Qur'ani ni aya hii:

يُوصِيكُمُ ٱللَّهُ فِيٓ أَوۡلَٰدِكُمۡۖ لِلذَّكَرِ مِثۡلُ حَظِّ ٱلۡأُنثَيَيۡنِ

**"Mwenyezi anawausia juu ya watoto wenu; fungu la mwanamume ni kama fungu la wanawake wawili….." (4:11)**

Kanuni hii ya jumla ndani ya Qur'ani kuhusu mtoto wa kiume kurithi mara mbili ya kiwango cha msichana imewekewa mipaka katika hadithi kwamba mtoto wa kiume ambaye amewauwa wazazi wake huwa harithi kabisa.

**3.3 Kuweka masharti (*al-taqiid* - التقييد)** Hii ni fatwa ambayo imetungiwa sheria ndani ya Qur'ani kwa namna isiyo na masharti lakini ikawekewa masharti na Sunnah. Mfano wa Qur'ani ni aya hii ifuatayo:

وَٱلسَّارِقُ وَٱلسَّارِقَةُ فَٱقۡطَعُوٓاْ أَيۡدِيَهُمَا جَزَآءَۢ بِمَا كَسَبَا نَكَٰلٗا مِّنَ ٱللَّهِۗ وَٱللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٞ ٣٨

**"Na mwizi mwanamume na mwizi mwanamke, ikateni mikono yao; ni malipo ya yale waliyoyachuma. Ndiyo adhabu itokayo kwa**

**Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu Mwenye hekima. (5:38).**

Kanuni ya jumla ya kisheria ya kukata mkono imewekewa mpaka kwenye vidole tu katika hadithi kwa sababu kiganja ni hitajio la sajida.



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 57 9/9/2015 12:56:07 PM

# SOMO LA TISA

## MGONGANO KATI YA HADITHI MBILI

Hapa tunataka tuone ni nini cha kufanya wakati kukiwa na mgongano au kupingana (***al-ta'arudhwu* - التعارض**) kati ya hadithi mbili.[28] Kunapokuwa kuna hadithi mbili zinazogongana na moja ni sahihi na nyingine haikuthibiti, basi hakuna mgongano wa kweli kwa sababu hiyo ambayo haijathibiti sio halali kisheria na haiwezi kubatilisha au kukosoa hiyo iliyothibiti kuwa sahihi. Tatizo ni pale zote mbili zikitimiza masharti ya usahihi na kisha tukashangaa tukawa hatujui namna ya kumaliza mgongano huo kwa sababu haiwezekani kwamba zote zinatoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) au kwa Maimam (a.s.).[29] Katika hali kama hizo, ingawa hadithi zote mbili zimethibitishwa na zimesimuliwa kwetu na vyanzo vya kutegemewa, hatimaye vyanzo hivi vikawa sio maasum, na kwa hiyo vina uwezekano wa kukosea. Kwa hiyo moja ya hadithi hizo lazima ipendelewe na hiyo nyingine kuachwa kando.

[28] Inapasa kuzingatiwa kwamba panapokuwa na hadithi mbili ambazo ni ama za ujumla na maalum au yenye mipaka (masharti) na isiyo na mipaka, huwa haziko kwenye mgongano kwa kuwa matokeo ya jumla ya zote mbili yanaeleweka kwa urahisi kwa sheria za akili ya kawaida ya maongezi. Mgongano au kupingana kunakuwepo tu kama hadithi mbili haziwezi kuwekwa sambamba. Kwa maneno mengine, katika suala la mgongano, hadithi hizo mbili zinakosoana zenyewe na haziwezi kuchukuliwa kwamba zimesimuliwa na mtu mmoja huyo huyo.

[29] Wakati ambapo inawezekana tu kwamba hadithi zote mbili zinatoka kwa Maasumiin (a.s.) ni katika suala la *taqiyah* (kuficha imani sahihi) ambapo, kwa mfano, kwa ajili ya kuokoa maisha ya Muislamu, Imam (a.s.) anaweza kuwa amewaagiza kuwa katika hali ambayo kwamba madhehebu yao yatabakia hayajulikani. Katika hali kama hiyo, hadithi iliyotolewa kwa ajili ya taqiyah lazima iainishwe na kisha inaweza ikapuuzwa.

## Tiba ya Hadithi zinazogongana:

Katika kinachofuatia, kwanza tutagundua hukumu ya akili (**al-'aql - العقل**) na halafu tutaangalia kwamba ni tiba gani inayoweza kupatikana kutoka kwenye hadithi. Hukumu ya akili inaashiria kwenye kanuni ya msingi na hukumu ya hadithi inaashiria kanuni ya pili. Kanuni ya msingi ina maana kwamba kwanza kabisa tunataka kugundua ni tiba gani itakuwa ya busara au kimantiki ikiwa kama tutakabiliwa na mgongano kama huo katika mawasiliano ya mtu na hakuna muongozo maalum uliotolewa na mtu yeyote unaopendekeza ni lipi la kufanya. Hata hivyo kunaweza kukawa na miongozo maalum iliyotolewa na mzungumzaji mwenyewe (kwa upande wetu, ni Mtukufu Mtume na Maimam, rehema na amani ziwe juu yao wote, ndio washauri ni nini cha kufanya).[30]

**Hukumu ya akili:** Miongoni mwa wanachuoni kuna maoni namna mbili kuhusiana na hili:

1. Baadhi ya wanachuoni wana maoni kwamba hadithi zote zinazogongana zinapaswa kuachwa na ichukuliwe kwamba hakuna hadithi zipatikanazo kuhusu mada hiyo. Kwa hiyo wao wanarudisha tatizo hilo kwenye kanuni za vitendo (*al-usuul al-'amaliyyah*) ambazo tutazichunguza baadaye. Kundi hili la wanachuoni linahoji kwamba wakati hadithi mbili zinapogongana, zinadhoofishana na kubatilishana zenyewe, hivyo hakuna mojawapo inayoweza kutegemewa na kufanyiwa kazi. Wanazilinganisha hadithi na alama za barabarani. Wakati unapoendesha, kama ukifikia alama inayoonyesha njia inayoelekea kwenye mji fulani unaweza ukaifuata hiyo. Hata hivyo, kama utaona alama mbili zina-

[30] Katika hali kama hizo ambamo miongozo maalum imewekwa na mzungumzaji bila shaka huchukua kipaumbele, kumaliza mgongano na bila kuacha nafasi kwa hukumu ya mantiki ya jumla.



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 59 9/9/2015 12:56:07 PM

zoelekeza pande tofauti kwa ajili ya mji huohuo, basi itakuwa kama hakukuwa na alama yoyote kwa sababu utakuwa hujui ni njia ipi ambayo ungepaswa kuifuata kati ya mbili hizo.

2. Kundi dogo la wanachuoni linashikilia maoni ya kwamba kunapokuwa na hadithi mbili zinazogongana, mtu anakuwa na hiari ya kufuata hadithi yoyote kati ya hizo kwa sababu kwa ubainifu wa taswira, kila upande wa mgongano unakuwa uko sahihi kwa wenyewe.

**Hukumu za Hadithi** – Hadithi zinatofautisha kati ya aina mbili za mas'ala:

1. Mas'ala ambamo mnakuwemo na vipaumbele: Kwa mujibu wa hadithi juu ya mgongano wa baadhi ya hadithi, kama kuna manufaa katika upande mmoja wa mgongano, upande huo utapendelewa na kufanyiwa kazi. Manufaa au ubora uliotatajwa katika hadithi ni kama yafuatayo:

- Umaarufu miongoni mwa wasimuliaji
- Makubaliano na Qur'ani na Sunnah
- Umbali na maoni ya wasiokuwa Shi'ah.[31]

Upendeleo huo hapo juu unatajwa katika hadithi mashuhuri sana inayoitwa: "Maqbuula ya Umar bin Hanzalah."[32] Sehemu ya hadithi hiyo inatolewa tena hapa chini:

---

[31] Hii linaleta uwezekano wa hadithi kuwa imebuniwa au kutamkwa katika hali ya Taqiyah bila mwelekeo kabisa au hata kutowezekana.

[32] Maqbuulah ni aina ya hadithi ambayo haitimizi masharti ya usahihi lakini wanachuoni wa zama zilizopita wameifanyia kazi (kwa hiyo tunaweza tukachukulia kwamba wao walikuwa na namna ya ushahidi uliopendekeza usahihi wake, ambao ushahidi huo kwa sasa haupatikani kwetu siku hizi). Umar bin Hanzalah alikuwa anatokea Kufah na anatambuliwa na kuthibitishwa na wanachuoni kama Shahiid al-Thaani na mwanawe.

"Imam (a) aliulizwa: "Katika suala la Shi'ah wawili wakijadili juu ya suala fulani je, liamuliwe vipi jambo hilo?" Imam (a) akajibu kwamba anapaswa kutafutwa msuluhishi na uamuzi wake lazima ufuatwe. Kisha Imam (a) akaulizwa: "Itakuwaje iwapo Shi'ah wawili watatafuta wasuluhishi wawili tofauti ambao wanatoa uamuzi unaopingana kwa kutumia hadithi tofauti?" Imam (a.s.) akajibu kwamba yule msuluhishi ambaye ni mwadilifu zaidi, mwenye elimu zaidi na mwaminifu zaidi katika maneno na mchamungu zaidi ndiye ambaye uamuzi wake lazima ufuatwe.

Imam (a.s.) alipoulizwa: "Itakuwaje wakati kama wasulihishi wote wana kiwango kimoja?" Imam (a.s.) akajibu kwamba basi hapo mtu anapaswa kuangalia ile hadithi walioirejea hao wasuluhishi ili kupata uamuzi. Mtu anapaswa kumfuata msuluhishi ambaye ametumia hadithi ambayo ni maarufu sana na ambayo inakubaliwa na watu wetu. Kisha Imam (a.s.) akaulizwa: "Ni vipi endapo kama wote wametumia hadithi maarufu na zilizosimuliwa kutoka kwa watu waaminifu?" Imam (a.s.) akajibu kwamba, hapo basi mtu anapaswa kuangalia hadithi zinazokubaliana na Qur'ani na Sunnah na zinazotofautiana na maoni ya wasiokuwa Shi'ah ili kuweza kuzifuata hizo.

Kisha Imam (a.s.) aliulizwa: "Basi itakuwaje kama hadithi zote zinakubaliana na Qur'ani na Sunnah, lakini mojawapo ikawa inakubaliana na maoni ya wasiokuwa Shi'ah na nyingine inatofautiana nao?" Imam (a.s.) akajibu: "Hiyo ambayo haikubaliani na maoni ya wasiokuwa Shi'ah inahusisha uongozi." Katika kujibu swali linalouliza kwamba kufanyike nini endapo hadithi zote zinakubaliana na maoni yao, Imam (a.s.) alisema: "Mtu anapaswa kuangalia ni ipi inayopendelewa sana na watawala na mahakimu wao ili aweze kutupilia mbali hiyo."

Katika kujibu swali linalouliza kwamba kufanyike nini endapo hadithi zote zinapendelewa na watawala wao, Imam (a.s.) alijibu

akasema: “Mtu anapaswa kuangalia ni ipi inayopendelewa sana na watawala na mahakimu wao ili aweze kuiweka pembeni.” Kisha Imam (a.s.) akaulizwa: “Itakuwaje kama hadithi zote zina mlingano na maoni ya watawala wao?” Imam (a.s.) akajibu akasema: “Basi hapo simameni mpaka mumuone Imam wenu, kwa sababu ni bora kusimama kuliko kuingia kwenye jambo ambalo litaharibu imani yako.”

Kwa hiyo, kutokana na hadithi hiyo hapo juu, vigezo vilivyotolewa na Imam (a.s.) kwa ajili ya kukubali mojawapo ya hadithi zinazogongana ni:

I. Hadithi iwe inajulikana vema – ni mashuhuri

II. Hadithi iwe inakubaliana na Qur’ani na Sunnah

III. Hadithii iwe kinyume na maoni ya wasiokuwa Shi’ah

IV. Hadithi iwe haipendelewi na watawala.

Suala linajitokeza la iwapo vigezo hivi vinapaswa kuchukuliwa kwa mpangilio uleule uliotajwa kwenye hadithi hii au hapana. Hapa tena wanachuoni hawakubaliani, baadhi yao wanasema kwamba mpangilio huo sio muhimu na wengine wanasema mpangilio huo ni muhimu.

Kunaweza pia kukawa na upendeleo ambao unaweza kutumika kuamulia usahihi wa hadithi lakini hazikutajwa katika kuamulia usahihi wa hadithi. Kwa mfano, tunaweza tukafanya utafiti juu ya wasimuliaji wa hadithi zote ili kuona iwapo kama mmojawao alikuwa na kumbukumbu nzuri zaidi au aliishi karibu sana na Maimam (a.s.). Kwa kuhitimisha, inaweza ikasemwa kwamba baada ya uchunguzi wa jumla wa vipaumbele vyote, mafaqihi wanapaswa kufanya maamuzi yao kwa mujibu wa hadithi iliyo karibu zaidi (*al-aqrab*) na ukweli.

**Mas’ala ambamo hamna kipaumbele:**

Pia kuna kutokukubaliana kuhusu uelewa wa maagizo yanayotolewa ndani ya hadithi.

1. Kundi la wanachuoni wanaelewa kutoka kwenye maagizo yanayotolewa katika hadithi kwamba katika kugongana kwa hadithi, faqihi ana hiari ya kuchagua yoyote kati ya hadithi mbili hizo na kutoa fatwa kama ipasavyo.
2. Kundi jingine la wanachuoni linaelewa kutoka kwenye maagizo yanayotolewa ndani ya hadithi kwamba endapo kunakuwa na hadithi mbili zinazogongana, basi zote kwa hali hii zinakuwa ni batili na faqihi hawezi kutoa fatwa kwa mujibu wa hizo, bali yeye mwenyewe anapaswa kutenda kwenye upande wa tahadhari. Kwa mfano: Kama kuna hadithi mbili, moja inasema kwamba unapaswa kuswali swala iliyofupishwa (qasr) na hiyo nyingine inasema unatakiwa kuswali swala kamili – faqihi hawezi kutoa fatwa juu ya hadithi hizi bali hasa yeye na wafuasi wake wanapaswa kutekeleza swala kwa namna zote kwa kuchukua tahadhari ya juu kabisa.
3. Kundi la tatu la wanachuoni linaelewa kutoka kwenye maagizo yatolewayo ndani ya hadithi kwamba endapo kunakuwepo na hadithi mbili zinazogongana, basi faqihi anaweza akatoa fatwa kulingana na hadithi ambayo inakaribia sana kwenye tahadhari.

# SOMO LA KUMI

## MAKUBALIANO (*AL-IJMAI*)

Wanachuoni wa Shi'ah wanaielezea ijmai kama ni makubaliano miongoni mwa kundi la wanachuoni, kundi mojawapo likiwa ni lile la Ma'sumiin, kama vile Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) au Maimam (a.s.). Hii ni kwa sababu wakati wote kunakuwa na uwezekano kwamba mwanachuoni wa kawaida atafanya kosa. Kwa hiyo, kwa mujibu wa Uislamu wa Shi'ah, makubaliano (ijmai) yanashushwa na Sunnah. Vilevile kama ushahidi wa ziada, baadhi ya wanachuoni wa Shi'ah wamesema kwamba wakati wowote kunapokuwa na makubaliano miongoni mwa wanachuoni wa Shi'ah katika wakati wa ghaib, tunaweza tukaamua kwamba Imam Mahdi (a.t.f.s.) lazima atakuwa ameidhinisha maoni yao, vinginevyo angeuokoa ummah kutokana na kushikilia nafasi ya makosa iliyochukuliwa na wote. Imam (a.t.f.s.) anaweza kuingilia kati, pengine kwa kuingiza wazo kwenye kichwa cha mwanachuoni mmoja au zaidi, ili kusije kukawa na makubaliano ya jumla juu ya nafasi yenye makosa.

Wanachuoni wa Sunni wanaielezea ijmai kama ni makubaliano miongoni mwa Waislamu wote au wale wa tabaka la wasomi (*ahl al-hall wa al-aqd*) wakinukuu hadithi kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) isemayo: "Ummah wangu kamwe hautakubaliana kwa pamoja juu ya jambo ambalo ni lenye makosa." Kwa nyongeza ya tatizo lililopo kwenye sanadi ya wapokezi wa hadithi hii, kuna tatizo baya kabisa ambalo ni kwamba kwa kawaida haiwezekani kuwapata

Waislamu wa madhehebu zote tofauti, wakaweza kukubaliana kwenye jambo lolote ambalo kwamba hakuna rejea ya aya ya wazi ya Qur'ani au ya hadithi.[33] Kwa hiyo, kwa wote Shi'ah na Sunni ni vigumu sana kuwa na makubaliano ya kweli kabisa kiutendaji mahali ambapo hakuna rejea katika Qur'ani au Sunnah.

## UAINISHAJI WA MAKUBALIANO

Kuna aina mbili za makubaliano (*ijmaa*):

a. Makubaliano yaliyopatikana (***al-ijmaa' al-muhassal*** – الاجماع المحصَل): Hii ni ijmai ambayo kuwepo kwake kunahakikishwa na kuthibitishwa na mafaqihi wenyewe.

b. Makubaliano yaliyosimuliwa (***al-ijmaa' al-manquul*** – الإجماع المَنقول**):** Hii ni ijmai ambayo kuwepo kwake kunahakikishwa na kuthibitishwa na wengineo.

Wanachuoni wa Shi'ah wanaamini kwamba hii aina ya pili ya makubaliano sio halali kisheria kwa sababu haisaidii kwenye uhakika na kila faqihi anapaswa kufikia uamuzi kutoka kwenye uchunguzi wake mwenyewe.

## UHUSIANO KATI YA IJAMAI NA SUNNAH:

Uhalali wa ijmai ni kwamba ni njia ya kugundua Sunnah, kama vile tu kwa "hadithi iliyosimuliwa kwa wingi (***al-khabar al-mutawaatir*** – الخبر المتواتر). Tofauti kati ya ijamai na Sunnah ni kwamba Sun-

[33] Ni dhahiri kwamba wakati wowote inapokuwepo rejea aya ya Qur'ani au hadithi juu wa wazo fulani kutakuwa hakuna haja ya makubaliano – *Ijmaa'*



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 65 9/9/2015 12:56:07 PM

nah ina asili ya kilugha na kwa hiyo inaweza kuashiria jambo kwa ujumla wake au kutokuwa kwake na masharti, ambapo ijmai sio ya kilugha na inabidi kuchukuliwa katika njia ndogo.[34]

[34] Kwa mfano: Katika mas'ala ya Zaka kuna hadithi zinazoelezea kwamba inaweza kutumika kwa malengo ya misaada ya sadaka. Hii inachukuliwa kama kanuni ya jumla na kwa hiyo faqihi ana uhuru mkubwa mwingi katika utumiaji wa Zaka. Hata hivyo, kama hamna ujumla wa kilugha na kutoka kwenye ijmaa' tuna kwa mfano kwamba, nusu ya khums inaweza kutumika katika mambo ambayo yatamridhisha Imam wa 12 (a.t.f.s.), faqihi anapaswa kuwa mwangalifu na awe na uhakika kabisa kwamba kwa lengo lolote lile atakalotumilia khums, linakubalika moja kwa moja kwa Imam wa 12 (a.t.f.s.).



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 66 9/9/2015 12:56:07 PM

# SOMO LA KUMI NA MOJA

## AKILI

Kila uamuzi wa kiakili ambao unaongozea kwenye uhakika kuhusu fatwa ya kidini unajulikana kama uthibitisho wa kiakili (***Daliil al-'aql* – دليل العقل**). Kwa mfano: Mwenyezi Mungu anapotuamuru kufanya kitendo na tunajua, kwa kutumia akili, kwamba ili kutekeleza wajibu huu tunahitaji kutimiza masharti fulani ingawa hayakutajwa katika amri hiyo. Kwa mfano, kutekeleza wajibu wa Hija tunalazimika pia kupata hati ya kusafiria (passport), tiketi za ndege, viza na kadhalika.

**Uwezo wa Akili:** Uwezo wa akili ni wa dhahiri kabisa na unaojidhihirisha wenyewe kiasi kwamba hauhitajii ushahidi wowote wa ziada. Ni kupitia matumizi ya akili ndipo tunaithibitisha dini yenyewe. Qur'ani tukufu pia inasisitiza matumizi ya akili. Kwa hiyo, wakati wowote tunapofanya uamuzi wa maana kibusara, tunaweza tukawa na uhakika kwamba unakubaliwa na Uislamu, kwa sababu Mwenyezi Mungu swt. ameiumba akili ili kutumika kwa madhumuni haya.

**Mgawanyo wa Hukumu za Kiakili:** Hukumu za kiakili zinagawanyika kwa mapana sana katika makundi makuu mawili ambayo halafu yake yanagawanyika katika makundi madogo madogo. Hayo makundi makuu mawili ni haya:

– Hukumu Huru ya Kiakili (***al-mustaqillaat al-'aq-liyyah* –** المستقلات العقلية)

- Hukumu Tegemezi ya Kiakili (***ghayr al-mustaqlat al-'aqliyyah*** **– غير المستقلات العقلية)**

1. **Hukumu Huru ya Kiakili:** Katika uamuzi au hitimisho lolote tunahitaji dhana mbili, dhana kuu na dhana ndogo. Kama dhana zote hizi mbili zinapatikana kupitia kwenye matumizi ya akili, basi hii inaitwa "hukumu huru ya kiakili." Mfano wa hili ni kama ifuatavyo:

- Dhana ndogo – Haki kibusara ni nzuri
- Dhana Kuu – Kila kilicho kizuri kibusara vilevile ni kizuri kidini pia.

Kwa hiyo haki ni nzuri kidini.

Hii ni hukumu ya kiakili hasa, kwa sababu dhana zote mbili, ile kuu na ndogo zimepatikana kupitia akili. Hukumu hii inasisitizwa vilevile katika dini.[35]

**Hukumu Tegemezi ya Kiakili:** Hii ni hukumu ya kiakili ambayo imetegemea kwenye hukumu ya kidini na kwa hiyo sio hukumu huru ya kiakili. Ni kupitia matumizi ya akili tunajua kwamba wakati wowote jambo linapoamriwa na Shariah, masharti yake pia yamehusishwa katika amri hiyo. Kwa mfano: Hija ni wajibu (ni hukumu ya kidini), na viza inahitajika (ni hukumu ya kiakili). Kwa hiyo, kupata viza ni wajibu.

Katika hukumu za kiakili, kanuni kubwa na ya msingi ni kanuni ya uhusika namna mbili (*qaa'idat al-mulaazamah*). Kwa mujibu wa kanuni hii, uamuzi wowote unaofanywa na akili, unafanywa

[35] Kama tunaweza kuielewa hukumu kwa akili zetu na hukumu hiyohiyo ikawa imetajwa katika vyanzo vya kidini, hii haina maana kwamba hiyo hukumu ya kiakili sio huru; bali hiyo hukumu ya kidini ni kwa kusisitizia kile ambacho tayari tumekijua. Kwa mfano: Tunatambua kiakili kwamba ni lazima tumtii Mwenyezi Mungu swt. au Mtume Wake (s.a.w.w.). Kwa hiyo tunapokuta maandiko kama haya yafuatayo: "Na mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume Wake!," tunatambua kwamba hili ni kutilia mkazo na kusisitiza umuhimu wa amri za kiakili.



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 68 9/9/2015 12:56:07 PM

na dini pia na uamuzi wowote uliofanywa na dini umefanywa na akili vilevile. Katika hukumu huru ya kiakili, uhusika namna mbili (*qaa'idat al-mulaazamah*) unahusisha wema na ubaya wa kiakili.[36]

[36] Ili kupata uwelewa au ufahamu mzuri wa aina hii ya hukumu ni lazima tuijadili dhana ya wema na ubaya (au uovu). Kuna idadi kadhaa ya ufafanuzi wa wema na uovu:

i) Yale mambo ambayo yanapendeza ni mazuri na yale ambayo hayapendezi ni mabaya. Mfano wa hili ni kwamba harufu inayopendeza ni nzuri ambapo sauti kubwa isiyopendeza ni mbaya. Wanachuoni wote wanakubaliana kwamba kwa ufafanuzi huu, kila mtu anaweza akatambua nini ni wema na nini ni uovu.

ii) Yale mambo yanayoelekezea kwenye ukamilifu ni mazuri na yale yanayoelekezea kwenye dosari ni maovu. Mfano wa hili ni, elimu ni nzuri kwa sababu inatuelekeza kwenye ukamilifu ambapo ujinga ni uovu kwa sababu unatuelekezea kwenye kutokukamilika. Wanachuoni wote wanakubaliana kwamba kwa maelezo haya vilevile, mtu anaweza akajua upi ni wema na upi ni uovu.

iii) Yale mambo ambayo yanastahili kusifiwa au kulaumiwa, yaani yale mambo ambayo kimaadili ni mazuri au ni mabaya. Mfano wa hili ni kwamba kuwa mkweli ni vizuri kimaadili, kwa hiyo huo ni wema, na kudanganya kimaadili ni vibaya kwa hiyo huo ni uovu. Kuna kutokukubaliana kati ya wanachuoni kuhusu iwapo kama aina hii ya wema na ubaya inakuwepo katika uhalisia au inakuwepo tu kwa sababu ya dini.

Ash'ariih wanaamini kwamba hakuna ukweli katika aina hii ya wema na uovu na kwamba inachukuliwa tu kwamba ni wema na uovu kwa sababu Mwenyezi Mungu amependa iwe hivyo. Kwa hiyo, wao wanasema kwamba chochote kile Mwenyezi Mungu anachokifanya ni wema, hata kama Yeye angekuwa amuingize muumini mchamungu Jahannam. Kadhalika, kama Yeye swt. angekuwa amuweke Peponi mtu muovu, asiyekuwa muumini - kafiri, bado itakuwa ni wema. Kwa mujibu wa maoni haya, wema na uovu sio mambo ya uhalisia kwa yenyewe bali yanategemea tu juu ya hiari ya Mwenyezi Mungu.

Maoni haya ya Ash'ari yanajulikana katika fikra ya Kiislamu kama "Wema na Uovu wa Kidini" (*al-tahsiin wa al-taqbiih al-Shar'iiyah* – التحسين و التقبيح الشرعان) na huko magharibi yanajulikana kama "Nadharia ya Amri ya Mungu."

Shi'ah na Mu'tazila wao hawakubaliani na maoni haya ya Ash'ari. Wao wanasema kwamba wema na uovu vipo kama ukweli halisi na kwamba hata bila kuwepo dini, bado kuna wema na uovu. Wanaamini vilevile kwamba Mwenyezi Mungu anatenda kulingana na uhalisia huu na hivyo Yeye swt. hatendi jambo ambalo ni ovu na kwamba kila kitendo ambacho Yeye swt. anakitenda kwa ukweli ni chema kwa uhalisia wake. Sio jambo la kiholela lisilo na msingi kwamba Mwenyezi Mungu anatutaka sisi kuwa wakweli, au wapole au wachamungu. Maoni haya ya Shi'ah na Mu'tazilah yanajulikana kama "Wema na uovu wa kiakili" (*al-tahsiin wa al-taqbiih al-'aqliiyan* – التحسين والتقبيح العقليان).

Kama tuna maoni kwamba wema na uovu ni kweli, basi inawezekana kuwa na hukumu za kiakili kama vile tu tulivyo na hukumu za kidini.

Katika hukumu tegemezi za kiakili, uhusika wa namna mbili unahusisha utoshelezaji, masharti ya wajibu huo, kinyume chake, mchanganyiko wa amri na makatazo na uingizaji wa ubatilishaji kwa makatazo.

## 1. KUTOSHELEZA:

Kutosheleza (*al-ijzaa* - الاجزاء) ni utekelezaji wa kivitendo wa hukumu moja ambayo inatosheleza kwa ajili ya hukumu nyingine. Kwa mfano: Kama mtu anafanya tayammam badala ya kutawadha kwa sababu ya kukosekana maji na kisha baada ya swala hiyo kukamilika anayapata maji, je ni lazima achukue udhu na kuiswali tena upya swala hiyo? Hukumu ya utoshelezaji inasema: "Hapana" kwa sababu tayammam ilitosheleza kwa ajili ya udhu.

Katika hukumu yoyote ya kidini, ubora ni kutekeleza ile hukumu halisi ya awali (*al-hukm al-waaqi'i al-awwalii* – الحكم الواقعي الاولى ) lakini katika mazingira yasiyo ya kawaida hili linaweza kuwa haliwezekani na kwa hiyo basi inatubidi kukimbilia kwenye hukumu halisi ya upili (*al-hukm al-waaqi'i al-thaanawii* – الحكم الواقعي الثانوي ). Katika hali hii, ile hukumu ya upili inatosheleza kwa ajili ya ile hukumu ya awali na kwa hiyo kama ikiwa inawezekana kutekeleza ile hukumu ya awali baada ya kukamilika kwa wajibu sio lazima kutekeleza wajibu huo tena. Hii ndio sababu ya kwa nini tayammam (hukumu ya upili) katika hali ya kutoweza kuchukua udhu (hukumu ya msingi) inatosheleza kwa ajili ya kuswali na hata kama baadaye ikiwa inawezekana kuchukua udhu, inakuwa sio lazima kurudia swala hiyo.

Wanachuoni wote wanakubaliana kwamba hakuna haja ya kurudia kitendo baada ya kukamilika kwa sababu kupitia hizi hukumu za upili Mwenyezi Mungu swt. amerahisisha wajibu juu



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 70 9/9/2015 12:56:07 PM

yetu na itakuwa ni kinyume na rehema Zake kutufanya turudie kitendo hicho. Qur'ani inaelezea katika aya ifuatayo:

يُرِيدُ ٱللَّهُ بِكُمُ ٱلْيُسْرَ وَلَا يُرِيدُ بِكُمُ ٱلْعُسْرَ

**"Mwenyezi Mungu anawatakia wepesi, wala hawatakii uzito….." (2:185).**

Lakini katika suala la kukosekana elimu ya hukumu halisi, mtu anapaswa kufuata hukumu ya dhahiri (*al-hukm al-dhaahirii* - الحكم الظاهري). Katika tukio kama hili, kuna kutoelewana kati ya wanachuoni kuhusu iwapo ile hukumu inayotumika inatosheleza kwa ajili ya hukumu halisi. Yaani kama elimu ya hiyo hukumu halisi ikithibiti, je itakuwa ni lazima kurudia kitendo hicho au hapana.

Maoni yaliyotawala ni kwamba hukumu inayotumika huwa haitoshi kama hukumu halisi ikija kujulikana na kitendo hicho itabidi kirudiwe tena kwa mujibu wa hizo taarifa mpya. Kwa mfano: Kama mtu amechukua udhu wakati wa asubuhi na inapofikia wakati wa swala ya mchana anakuwa hana hakika kama udhu huo ungali upo, kwa mujibu wa *al-istishaab* (aina ya hukumu inayotumika), mtu huyo anaweza kuchukulia kwamba udhu huo bado unafanya kazi na akaanza kuswali. Hata hivyo, kama baadaye atakumbuka kwamba udhu huo kwa kweli ulikwisha batilika, basi ni lazima airudie swala hiyo.

**Hitimisho:** Kufanya mukhtasari wa hayo yaliyosemwa hapo juu, tunaweza kuhitimisha kama ifuatavyo:

i. Hukumu halisi ya upili inatosheleza na hakuna haja ya kurudia tena kitendo hicho iwapo ile hukumu halisi ya awali itathibiti baada ya kitendo.



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 71 9/9/2015 12:56:07 PM

ii. Kwa mujibu wa wengi wa wanachuoni, sheria inayotumika huwa haitoshelezi na kwa hiyo kitendo hicho kinapasa kurudiwa endapo ile hukumu halisi itathibiti baada ya kitendo.

## 2. KITANGULIZI CHA YALIYO WAJIBU

Kitangulizi cha yaliyo wajibu (*muqaddimat al-waajib* – مقدمة الواجب) ni kitendo chochote ambacho kukitenda kwake kunahitajika kwa ajili ya utekelezaji wa kile cha wajibu.[37] Mifano ya masharti ya yaliyo wajibu ni udhu kwa ajili ya swala au kupata viza kwa ajili ya Hija. Hii ni kinyume na kitangulizi cha kitu kuwa wajibu (*muqaddimatul-wujuub*) ambalo ni jina la jumla kwa ajili ya kitendo chochote ama hali ambayo kuwepo kwake kunahitajika kwa ajili ya wajibu huo kutekelezeka, kama vile kubalehe na kuwa na akili timamu na kadhalika.[38] Kwa maneno mengine, katika hali ya hilo la awali, wajibu unakuwepo na vitangulizi pia vinakuwa ni wajibu kwa sababu hali halisi ya wajibu wa kitendo chenyewe. Hata hivyo, katika hali ya hili la baadaye hakuna wajibu wenye nguvu bila ya vitangulizi hivyo na kwa hiyo hakuna wajibu wa kulazimu kuvileta vitangulizi hivyo.

Vitangulizi vya wajibu vinagawanya zaidi katika namna mbili zifuatazo:

- **Vitangulizi vya ndani vya yaliyo wajibu (*al-muqaddimatul-daakhiliiyah*)** – Kitangulizi chochote muhimu ndani ya kitendo hicho, kwa mfano, katika swala, ule utekelezaji wa visomo, rukuu na sajida.

[37] *Muqaddamat al-waajib* inaitwa pia *al-muqaddimat al-wujuudiiyah* ambayo kilugha ina maana ya kitangulizi kinachosisitiza au kutilia mkazo. Sababu ya kulipa jina hili ni kwamba kuwepo kwake kunahitajika kwa ajili ya kuwepo kwa lile ambalo ni wajibu.

[38] Vitangulizi vya wajibu vinaweza kuwa vya jumla kama vile balehe na kuwa na akili timamu au maalum kwa ajili ya wajibu fulani kama vile uwezo wa kidini kwa ajili ya Hija kufanywa kuwa ni wajibu.



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 72 9/9/2015 12:56:07 PM

- **Vitangulizi vya nje vya yaliyo wajibu (*al-muqaddimatul-kharijiiyay*)** – Kitangulizi chochote cha nje ya kitendo kama vile udhu ambao kufanyika kwake kunahitajika kabla ya kuanza kuswali.

Kitangulizi cha nje cha yaliyo wajibu baadaye kinagawanywa kwa mara mbili zaidi:

I. Kitangulizi cha nje cha kiakili cha wajibu: Vitangulizi hivi vinaweza kueleweka kupitia akili kama vile kupata viza kwa ajili ya kwenda kuhiji.

II. Kitangulizi cha nje cha wajibu cha kidini: Vitangulizi hivi vinaweza kutambulika kupitia dini kama vile kuelekea Ka'aba na kuwa na twahara kwa ajili ya kusimamisha swala.

Kwa nyongeza ya majina hayo hapo juu, baadhi ya vitangulizi huwa vinapewa majina maalum:

**Kitangulizi kinachofuta (*al-muqaddimatul-mufawwitah* – المقدمة المفوتة):** Aina hii ya kitangulizi ni lazima itumike kabla ya wakati wa kitendo kuingia, kama vile kusafiri kwenda Makkah kabla ya wakati wa Hija au kuoga josho la twahara kabla ya alfajiri katika mwezi wa Ramadhani. Kushindwa kuleta vitangulizi kama hivi kwa wakati muafaka kunafuta ule uwezekano wa kutekeleza huo wajibu.[39]

[39] Wajibu wa aina hii ya kitangulizi unaweza kueleweka kwa kutumia akili kwa sababu kama Mwenyezi Mungu swt. amelifanya jambo kuwa ni wajibu juu yetu katika muda maalum, basi ni lazima tuwe tayari kutekeleza wajibu huo katika wakati huo maalum, hivyo basi, maandalizi yote lazima yawe tayari yamekwisha kufanyika kabla ya wakati huo husika.

Kwa mfano, kama tunataka tupate chakula cha mchana wakati wa saa sita kamili, basi mapishi lazima yafanyike kabla ya hiyo saa sita ili kuweza kula chakula cha mchana ifikapo hapo saa sita kamili ya mchana.

**Kitangulizi cha kiibada (*al-muqaddamatul-ibaadiiyah* – المقدمة العبادية):** Hii ni aina ya kitangulizi cha kidini ambacho utekelezaji wake sahihi unahitaji nia thabiti. Kwa maneno mengine, ni lazima kifanyike kwa ajili ya Mwenyezi Mungu swt. hivyo kitangulizi chenyewe kinakuwa ni kitendo cha ibada.[40] Aina hii ya kitangulizi imewekewa mipaka kwenye udhu , josho na tayammam.

**Je, vitangulizi ni wajibu?**

Baada ya kuelewa ufafanuzi wa vitangulizi vya yaliyo wajibu na aina zake tofauti, sasa ni wakati wa kuchunguza maoni ya wanachuoni katika suala hili. Kwa kweli hakuna shaka kwamba vitangulizi vya yaliyo wajibu vyenyewe kiakili ni wajibu na ni lazima tuvilete au kusababisha. Hata hivyo, swali ni iwapo kama vyenyewe ni wajibu kidini au hapana. Matokeo ni kwamba, kama kitangulizi kinakuwa kidini ni wajibu, kutokileta kivitendo kwenyewe kutakuwa ni dhambi lakini kama wajibu kiakili tu kuacha kukileta hakutakuwa ni dhambi.

Lililo dhambi pekee katika hili suala la mwishoni ni kuacha kutenda lile tendo la wajibu lenyewe.

Hapa kuna mjadala. Wanachuoni wa hivi karibuni kabisa wameamua kwamba hakuna wajibu wa kidini wowote ulioambatanishwa kwenye vitangulizi kwa sababu kama jambo linaeleweka kupitia matumizi ya akili (katika suala hili, ule umuhimu wa kutenda hicho kitangulizi), basi hakuna haja ya kutunga sheria zaidi. Kwa hiyo, kama maandishi ya kidini yakiashiria umuhimu wa

[40] Hii ni kinyume na vitangulizi vingi ambavyo vinahitajika kwa ajili ya wajibu fulani kutekelezwa lakini ambapo hakuna manuizi yanayohitajika. Hivi vinaweza kufanywa na mtu kwa nia ya kupata ukaribu na Mwenyezi Mungu swt. au bila ya nia yoyote maalum akilini mwake, au kufanywa na mtu kwa niaba ya mtu mwingine. Mfano mmoja ni kuvaa nguo safi (toharifu) katika swala. Kama nguo zako sio safi, zinaweza kufuliwa na wengine kwa niaba yako, ama ukazifua wewe mwenyewe, bila manuizi ya kupata ukaribu na Mwenyezi Mungu.



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 74 9/9/2015 12:56:08 PM

jambo ambalo tayari tunalifahamu kwa kutumia akili zetu, litakuwa ni suala la msisitizo tu.

## 3. KINYUME CHAKE

Kwa kinyume, tunamaanisha kinyume cha kitendo kilichotolewa (***al-dhwid* - الضد**) Kuna aina mbili tofauti za kinyume:

1. **Kinyume Maalum (*al-lwid al-khaasw* – الضد الخاص):**Huu ni utekelezaji wa kitendo mbali na kile kilichoagizwa. Kwa mfano, kama msikiti unanajisiwa, tunaamrishwa kuusafisha, lakini kama tungekuwa tuswali katika sehemu nyingine ya msikiti huohuo bila ya kusafisha ile sehemu chafu, basi kitendo hiki cha kuswali hapo kinaitwa kinyume maalum (cha kusafisha).

2. **Kinyume cha Jumla (*al-dhwid – al-'aamm* – الضد العام)** Huku ni kuacha, yaani kushindwa kutekeleza kile ambacho kimeamrishwa. Kwa mfano, wakati tunapoamrishwa kusafisha msikiti, kama tutaacha kuusafisha hivihivi tu, kuacha huku au kushindwa kunaitwa kinyume cha jumla (cha kusafisha).

Swali hapa ni kwamba pale tunapoamrishwa na Mwenyezi Mungu kufanya jambo, je tunaweza kuamua kwamba kinyume cha jumla au cha maalum kimekatazwa au hapana? Wengi wa wanachuoni wanaamini kwamba kama tumeamrishwa kufanya jambo fulani basi kinyume chake cha jumla kidini kimekatazwa. Hata hivyo, kuna baadhi ya wanachuoni wanyofu ambao wanaamini kwamba kile kinyume cha jumla hakikukatazwa kidini. Wanachuoni hawa wanaamini kwamba kwa vile tunajua kwa akili zetu kwamba ni kosa

kuacha kufanya kile kilichoamrishwa, hakuna haja ya ukatazwaji wa kinyume cha jumla kwa nyongeza ya amri hiyo.

Hiyo imani juu ya kukatazwa kidini kwa kinyume maalum kunategemea kukubalika kwa katazo la kidini la katazo la jumla. Kwa hiyo wale wanaokataa hili la baadaye wanakataa lililotangulia kwa urahisi zaidi.

## 4. MCHANGANYIKO WA AMRI NA KATAZO:

Wakati mwingine mtu anaweza akakabiliana na hali ambamo amri zinazopingana mbili na makatazo zimejumuishwa pamoja. Kwa mfano, kuwa ndani ya nyumba ya mtu bila idhini yake. Hata hivyo, wakati ukiwa mahali hapo, kama wakati wa swala ukiwadia, hapo kuswali swala yako kunakuwa ni wajibu.[41] Kwa hiyo, katika kadhia hiyo moja kuna mchanganyiko wa katazo na amri (***Ijtimaa' al-amr wa al-nahy* – اجتماع الأَمر و النهي ).** Bila shaka migongano kama hiyo huwa haitokezi ila kwa bahati mbaya kutokana na uamauzi usio sahihi unaofanywa na watu wenyewe, sio na Mwenyezi Mungu swt.

Baadhi ya wanachuoni wanaamini juu ya uwezekano wa yote, amri na katazo kutumika. Kwa sababu hiyo, kama mtu atasababisha kile kilichoamrishwa basi atakuwa ametii kwa kuzingatia amri na ameasi kwa kuzingatia katazo.  Wapo wengine wanaoamini katika kutokuwezekana kwa yote, amri na katazo kubakia katika matumizi. Wanachuoni hawa wanaweza kutoa kipaumbele kwenye amri na kwa hiyo mtu anapaswa kutii hiyo amri na hakutaweza tena kuwa na katazo au wanaweza kutoa kipaumbele kwenye katazo  na kwa hiyo mtu anapaswa kufuata hilo katazo na kutakuwa hakuna haja

[41] Katika mfano huo hapo juu, tumechukulia kwamba kitangulizi cha swala cha mahali pa kuswalia kuwa kimeruhusiwa hakupo.



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 76 9/9/2015 12:56:08 PM

ya kuleta kile ambacho kimeamrishwa. Bado kuna wanachuoni wengine zaidi wanaotofautisha kati ya hali ambamo kuna mbadala au hapana na kati ya mas'ala ya hiari na isiyo ya hiari.

Kwa jumla kuna uwezekano namna tatu. Kwa mfano, katika suala la mchanganyiko wa wajibu kwa ajili ya swala na katazo la kuwa kwenye nyumba ya mtu mwingine bila ya idhini yake, kunaweza kukawa na mojawapo ya uwezekano huo wa aina tatu:

i. Unakuwepo mbadala – inawezekana kuondoka nyumbani hapo

ii. Hakuna chaguo mbadala, lakini upo ndani ya eneo bila ya kosa lako mwenyewe, kwa mfano, umefungwa katika sehemu iliyoporwa. Katika hali hii hakuna lawama juu yako.

iii. Hakuna chaguo mbadala lakini umo ndani ya eneo kwa makosa yako wewe mwenyewe na huwezi kutoka nje, ama kwa sababu umefungiwa ndani au hakuna muda wa kutosha. Katika hali hii wewe unahesabiwa umetenda dhambi.

Kutafakari juu ya hali hizo hapo juu, inaelekea kwamba kama kunakuwa na chaguo mbadala basi linabidi kuchukuliwa na kuswali kwenye eneo hilo hakutaruhusiwa kwa sababu kutenda kitendo cha ibada wakati unafanya dhambi hakuwezekani. Kwa vyovyote vile swala hiyo itakuwa batili. Lakini kama kitendo kilikuwa sio cha kiibada na kwa hiyo hakuna manuizi yoyote yaliyohitajika (kwa mfano, kufua nguo kwa ajili ya kuzifanya kuwa tohara ili kuweza kuswali nazo ukiwa umezivaa) hapo basi hakuna suala la uhalali.

Kuhusu hali zote ambazo ndani yake hamna mbadala wake, inaelekea kwamba swala ni halali kwa sababu ni kitendo tofauti na kile cha mwanzo (cha kuingia ndani ya nyumba).[42]

[42] Baadhi ya wanachuoni wanashikilia kwamba katika hali ambamo umo katika hali hii ya mashaka kupitia makosa ambayo sio yako binafsi, basi swala inakubalika. Hata



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 77 9/9/2015 12:56:08 PM

# 5. KUHUSISHWA UBATILISHAJI KWA KATAZO:

Swali hapa ni iwapo katazo kimantiki linahusisha kufasidi (***al-fasaad* - الفساد**) au hapana. Kwa maneno mengine, kuna faida yoyote katika kutenda kitendo kilichoharamishwa au kinakuwa ni batili na kisichofaa?

Suala hili linachunguzwa kwa namna mbili tofauti. Ya kwanza ni wakati kitendo kilichokatazwa ni kitendo cha ibada (***al-'ibaadah* - العبادة**) kama vile swala na saumu. Kwa mfano, imekatazwa kwa mwanamke kuswali wakati akiwa kwenye ada yake ya kila mwezi, au imekatazwa kufunga katika siku ya *Idd al-Fitr* au *Idd al-Udh'ha*. Katika masula kama hayo, makatazo yanakifanya kitendo hicho kuwa batili.

Namna ya pili ni wakati kitendo kinachokatazwa kinapokuwa ni kile ambacho sio cha kiibada (***al-mu'aamalah* - المعاملة**). Hapa kuna tofauti ya maoni kuhusu iwapo kama katazo linafanya kitendo kuwa batili. Mfano wa hili ni kule kukatazwa kufanya biashara wakati swala ya Ijumaa ikiwa inaendelea, kama ilivyotajwa kwenye aya ifuatayo:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ إِذَا نُودِىَ لِلصَّلَوٰةِ مِن يَوْمِ ٱلْجُمُعَةِ فَٱسْعَوْاْ إِلَىٰ ذِكْرِ ٱللَّهِ وَذَرُواْ ٱلْبَيْعَ ۚ
ذَٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ إِن كُنتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٩﴾

**"Enyi mlioamini! Ikinadiwa swala Siku ya Ijumaa, nendeni upesi kwenye dhikri ya Mwenyezi Mungu, na wacheni biashara. Hayo ni bora kwenu kama mnajua." (62:9).**

hivyo, katika suala ambalo mashaka yanatokea kutokana na vitendo vyako, hapo swala haikubaliki.



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 78 9/9/2015 12:56:08 PM

Sasa swali ni iwapo kama maafikiano hayo ni halali kama mtu anauza kitu wakati wa swala ya Ijumaa. Yaani kwamba, huyo mnunuaji anakimiliki hicho kinachouzwa au kinabakia ni mali ya muuzaji na je, pesa ile iliyolipwa kununua kitu hicho ni mali ya muuzaji ama bado inabakia kuwa ni mali ya mnunuzi?

Wanachuoni wote wanakubaliana kwamba katika hali kama hizo, manunuzi yenyewe ni halali kwa sababu kama manunuzi hayo hayo yangefanyika katika wakati wowote ule mbali na ule wa muda wa swala ya Ijumaa kusingekuwa na tatizo lolote ndani yake. Hivyo inaweza kuhitimishwa kwamba makatazo katika kadhia hii hayamaanishi ubatilishwaji. Hata hivyo, kama katazo lipo juu ya aina ya manunuzi yenyewe (na sio katika uendeshaji wa mapatano katika mazingira maalum) kama makatazo ya riba, basi makatazo hayo yanamaanisha ubatili.



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 79 9/9/2015 12:56:08 PM

# SOMO LA KUMI NA MBILI

## KANUNI TEKELEZI

Kama tulivyoona mapema katika kitabu hiki, hukumu tekelezi inakuja kutumika tu wakati kunapokuwa na shaka kuhusu ile hukumu halisi na katika suala hili kuna mazingira namna nne ambayo yataangaliwa kwa mpangilio. Wakati mwingine hali hiyo iliyotangulia inakuwa inajulikana na wakati mwingine haijulikani. Kama hali iliyotangulia inafahamika, basi tunatumia kanuni ya uendelevu (***al-istishaab* - الاستصحاب**). Laa sivyo, wakati mwingine huwa tunajua kwamba kuna wajibu uliowekwa juu yetu na wakati mwingine hatujui. Kama hatujui kwamba kuna wajibu unaotumika basi tunatumia ile kanuni ya uachwaji (***al-baraa'ah* - البراءة**). Kama tukijua kwamba wajibu huo unatumika, lakini tukawa hatujui kinaganaga chake, au jinsi ya kuutenda, basi wakati mwingine inawezekana kutenda kwa mujibu wa tahadhari na wakati mwingine haiwezekani kuutennda. Katika hiyo hali ya kwanza, tunatumia ile kanuni ya tahadhari (***al-ihtiyaat* - الاحتياط**) na katika hii hali ya baadaye tunatumia kanuni ya hiari (***al-takhyiir* - التخيير**). Hii ni wakati kunapokuwepo na majukumu mawili yanayopingana, na kwa hiyo hakuna njia ya kuhakikisha kwamba mtu ameyatekeleza yote.

### Kanuni ya Uendelevu

Kwa Kiarabu, istis'haab kilugha ina maana ya kuchukua kitu pamoja nawe, ili kuandamana nawe. Maana yake ya kiufundi ni kudhania kwamba ile hali iliyopita mwanzoni bado ipo inaendelea. Kudha-



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 80 9/9/2015 12:56:08 PM

nia uendelevu, ile hali iliyopita lazima ijulikane kwa uhakika wake na shaka pekee lazima iwe kwenye hali iliyopo tu kwa sasa. Kwa mfano, mtu ambaye kwa uhakika amechukua udhu wakati wa asubuhi lakini wakati wa swala za mchana anaweza asiwe na uhakika kwamba udhu ule bado upo unafanya kazi.[43] Katika suala kama hili, inaweza ikadhaniwa kwamba udhu huo bado ni halali.

Kwa kuhitimisha, ili kuthibiti uendelevu, mtu lazima awe na:

- Uhakika kuhusu hali iliyotangulia
- Kuwa na shaka na hali ya sasa
- Wakati wa shaka lazima uunganishwe na wakati wa uhakika
- Suala la shaka na uhakika lazima liwe ni moja lilelile.
- Yote, uhakika na shaka lazima yawe ni halisi
- Hali ya uhakika lazima iitangulie hali ya shaka.

### Hoja kwa ajili ya kanuni ya uendelevu

**Hoja ya kibusara:** Kwa mujibu wa baadhi ya wanachuoni, uendelevu ni jambo ambalo linatumiwa na watu wote wenye busara katika jamii zote na hivyo ni lazima ikubalike katika dini pia. Wao wanahoji kwamba, kama kwa mfano, unayo namba ya simu ya rafiki yako, lakini una shaka kuhusu iwapo rafiki huyo bado anaishi hapo au hapana, jibu la kibusara ni kudhania kwamba bado yuko hai na kujaribu kumpigia simu hapo. Wanahoji kwamba hili ni kweli hata kwa wanyama pia. Kwa mfano, wakati ndege wanaporuka kutoka kwenye viota vyao, wanarejea kwenye sehemu hiyo hiyo, hata baada ya msimu mmoja, wakidhania kwamba mahali pa viota vyao patakuwa bado papo.

[43] Hivyo, kama kuna shaka kuhusu iwapo kama udhu ulichukuliwa wakati wa asubuhi au hapana, basi uendelevu hauwezi kuthibiti.

**Hoja kutoka kwenye Hadithi:** Kuna hadithi kadhaa zinazoashiria uhalali wa kanuni ya uendelevu. Kwa mfano, inasimuliwa kwamba katika kujibu swali lililoulizwa na Ammar, Imam al-Kadhim (a) alisema: "Kama una shaka, tegemea juu ya lenye uhakika." Ammar akauliza: "Hii ni kanuni?" Imam (a) akajibu: "Ndio."[44]

Katika hadithi nyingine, Zuraarah alimuuliza Imam as-Sadiq (a) kuhusu mtu ambaye amechukua udhu lakini akawa na shaka kuhusu kama alilala baadaye au hapana. Imam (a) alijibu kwamba kwa sababu walikuwa katika hali ya shaka na hapo kabla walikuwa na uhakika, wanaweza kuchukulia kwamba ule uhakika (kuhusu udhu) ulikuwa bado upo mpaka watakapokuwa na hakika kwamba udhu wao umevunjika. Kisha Imam (a) akasema: "Yeye kamwe habatilishi uhakika kwa shaka, bali anabatilisha uhakika kwa uhakika mwingine."[45]

## KANUNI YA UACHWAJI:

Kuna aina mbili za uepukaji (baraa'ah) au uachwaji;[46] ile ya kidini na ya kiakili.

**Uachwaji wa kidini (*al-baraa'ah al-sha'iiyah* – البراءة الشرعية).** Kama kuna shaka kuhusu iwapo kama kuna wajibu au hapana, basi kwa mujibu wa vyanzo vya kidini, hakuna kinachomfunga mtu, na anakuwa huru kutokana na wajibu. Hata hivyo, kuna tofauti kati ya masuala ya mtu binafsi na masuala ya jumla. Kwa mfano, kama mtu hajui iwapo kwamba kipande fulani cha nguo au chakula kimenajisika

44 *Wasaa'il al-Shi'ah*, Mlango wa Nane katika milango juu ya *al-Khalal*

45 *Wasaa'il al-Shi'ah*, Mlango wa kwanza katika milango juu ya *Nawaaqid al-udhu*, no. 1

46 Inapasa kuzingatiwa hapa kwamba kwa uepukaji au uachwaji tunamaanisha ukanushaji wa wajibu. Hii ni tofauti na uachwaji katika maana yake ya kawaida, ambamo kwa uhakika mna wajibu, lakini mtu anaweza akasamehewa katika wajibu huo.

au hapana – hili ni suala la binafsi na hapa hiyo shaka inakuwa juu ya suala hilo (*al-shubhat al-misdaaqiiyah*), na sio hukumu yenyewe (*al-shubhat al-hukmiiyah*). Wanachuoni katika masuala ya binafsi wanasema kwamba hakuna uchunguzi unaohitajika. Hata hivyo, katika hali ya shaka kuhusu hukumu, mtu ni lazima achunguze na atafute kwenye vyanzo vya kidini ili kujua kama kuna wajibu au hapana, na kama mtu hatapata ushahidi juu ya wajibu, basi mtu anapaswa kutenda kwa mujibu wa kanuni ya uachwaji.

Hoja kwa ajili ya uachwaji wa kidini: Qur'ani Tukufu inasema:

"لَا يُكَلِّفُ ٱللَّهُ نَفْسًا إِلَّا مَآ ءَاتَىٰهَا ۚ سَيَجْعَلُ ٱللَّهُ بَعْدَ عُسْرٍ يُسْرًا ﴿٧﴾

**"Mwenyezi Mungu haikalifishi nafsi y oyote ila kwa kadiri ya alivyoipa. Mwenyezi Mungu atajaalia baada ya uzito wepesi." (65:7).**

Kwa hiyo, kama Mwenyezi Mungu swt. hakutujulisha sisi juu ya wajibu, hatutegemewi kutekeleza wajibu huo na wala hatuna hatia ya dhambi.

Hoja moja kutoka kwenye hadithi inarejelea kwenye kile ambacho kimesimuliwa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s):

> "Mambo tisa yamenyanyuliwa kutoka kwenye ummah wangu (ambayo kwayo hawatawajibishwa): kosa, usahaulifu, lile ambalo wamelazimishwa kulitenda, lile ambalo hawalitambui, lile ambalo hawana uwezo wa kulitenda, lile ambalo wamelazimika kulitenda, wivu (alimuradi umebakia ndani ya moyo kama husda na haufanyiwi kazi), kupatwa na dalili za kishetani, na kuangukia kwenye hali ya kutafakari juu ya minong'ono ya shetani juu yake



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 83 9/9/2015 12:56:08 PM

kuhusu asili ya maumbile, mradi tu inabakia katika moyo na haitamkwi wala kufanyiwa kazi."[47]

Kifungu cha maneno: "lile ambalo hawalitambui," kinarejelea kwenye kanuni ya uachwaji.

**Uachwaji wa Kiakili** (***al-baraa'ah al-'aqliiyah*** – البراءة العقلية) – Kwa kutumia akili zetu, tunajua kwamba kama bwana anamtaka mtumishi afanye kitendo fulani, ni lazima amfahamishe kuhusu hilo. Ubaya wa kuadhibu bila ya kutangazia kabla ni wazo ambalo linakubaliwa na mataifa yote kwa nyakati zote na katika sehemu zote na ndio msingi wa uachwaji.[48]

Ya usanifu wa hoja Ya ufunuo wa maarifa

## KANUNI YA TAHADHARI

Kuna aina mbili za tahadhari (*al-ihtiyaat*): ya kidini na ya kiakili.

**Tahadhari ya kidini** (***al-ihtiyaat al-shar'ii*** – **ا لاحتياط الشرعي**) – Tahadhari ya kidini imeegemea kwenye vyanzo vya kidini vinavyoashiria umuhimu wa kutenda kwa uangalifu na tahadhari ili kuhakikisha kwamba ule wajibu unaohusika unatiiwa.[49]

---

47 *Wasa'il al-Shi'ah*, Kitabu cha Jihadi ya Nafsi, Mlango wa 56, no. 1. Hapa "yamenyanyuliwa" ina maana kwamba haya ni mambo yanayoelezeka na kusahameheka na, Mwenyezi Mungu swt. hatauadhibu ummah kwa ajili ya mambo haya.

48 Shahid Sayyed M. Baqir al-Sadr anaamini kwamba ingawa maelezo hayo hapo juu ni kweli, hayawezi kusemwa kwa ajili ya wajibu wetu kwa Mwenyezi Mungu swt. kwa sababu uhusiano wetu na Yeye ni tofauti. Anasema kwamba sisi tumeumbwa na Mwenyezi Mungu na hatuna haki ya kuingilia uumbaji Wake. Ni kama kuwa ndani ya nyumba ya mtu kama mgeni na kisha ukabadilisha mapambo ya mandari ya nyumba bila idhini yw mwenyewe. Kwa hiyo Shaahid Sadr anaamini tu katika uachwaji wa kidini na sio katika uachwaji wa kiakili.

49 Wengi wa wanachuoni wanakubali kwamba kuna tahadhari ya kidini na wanaamini tu juu ya tahadhari ya kiakili chini ya mazingira fulani



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 84 9/9/2015 12:56:08 PM

**Tahadhari ya kiakili (*al-ihtiyaat al-'aqlii* – الاحتياط العقلي ) –** Wakati wowote tunapojua kwamba kuna wajibu juu yetu, ni lazima tuhakikishe kwamba tumeutekeleza wajibu huo. Kwa maneno mengine uhakika wa wajibu unahitajia uhakika wa utii. Njia nyingine ya kujadili juu ya tahadhari ya kiakili ni kurejea kwenye umuhimu wa kiakili wa kinga kutokana na uwezekano wa madhara. Mfano wa hili ni suala la nyumba yenye ujenzi usio imara – kunakuwa na uwezekano wa hatari. Hapa akili zetu zinatuambia tuondoke kwenye nyumba hiyo na tuchukue tahadhari.

## Kanuni ya Hiari

Kuna aina mbili za hiari (*al-takhyiir*): ya kidini na ile ya kiakili.

**Hiari ya kidini/kisheria (*al-takhyiir al-shar'ii* – التخيير الشرعي ):** Katika hali hii tuna hiari ya ni wajibu gani tuufuate. Katika hali kama hii, Mwekasheria Mwenyewe ametupa sisi hiari kati ya vipande viwili vya ushahidi vinavyopingana (al-amaarah) ambavyo vinatuongozea kwenye wajibu mbili zinazogongana, kama vile kuwa na hadithi mbili zenye msimamo mmoja na hukumu zinazogongana.

**Hiari ya kiakili (*al-takhyiir al-'aqlii* – التخيير العقلي):** Kwa mujibu wa akili, kama tuna amri mbili zinazopingana zinazoelekea zote kutoka kwa Mwenyezi Mungu, huwa tunajua kwamba hatuwezi kufuata zote pamoja. Hata hivyo, kwa sababu tunajua kwamba moja ya hizi bila shaka na kwa hakika inatoka kwa Mwenyezi Mungu, wala hatuwezi kuzipuuza vilevile. Hivyo tuna hiari katika kipi kimojawao kati ya vitendo hivyo viwili tukifanye. Kwa mfano, kama tuna shaka kuhusu iwapo kama jambo fulani ni wajibu au limekatazwa, hakuna njia ya kulifanya kwa mujibu wa tahadhari kwa sababu kama ni la wajibu, limekatazwa kutokulifanya, na kama limekatazwa basi ni



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 85 9/9/2015 12:56:09 PM

wajibu kutokulifanya. Kama hakuna njia ya kugundua ile hukumu halisi ya kweli, basi mtu anaweza kuchagua ni ipi kati ya hukumu mbili hizo anayopenda kuitekeleza.



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 86 9/9/2015 12:56:09 PM

## OORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu Ya Kwanza Mpaka Thelathini
2. Uharamisho Wa Riba
3. Uharamisho Wa Uwongo Juzuu Ya Kwanza
4. Uharamisho Wa Uwongo Juzuu Ya Pili
5. Hekaya Za Bahlul
6. Muhanga Wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo Iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab Vazi Bora
9. Ukweli Wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu Imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini Katika Swala
16. Misingi Ya Maarifa
17. Kanuni Za Ndoa Na Maadili Ya Familia
18. Bilal Wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi Wa Historia Ya Uislamu Na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an Na Hadithi
24. Elimu Ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu Ya Shia
26. Ukusanyaji Na Uhifadhi Wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo Kutoka Katika Qur'an
29. Uislamu Mfumo Kamili Wa Maisha Ya Kijamii
30. Mashukio Ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu Kwa Mujibu Wa Kitabu Na Sunna.
34. Haki Za Wanawake Katika Uislamu
35. Mwenyezi Mungu Na Sifa Zake
36. Kumswalia Mtume (S)
37. Nafasi Za Ahlul Bayt (A.S)
38. Adhana



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 87 9/9/2015 12:56:09 PM

39. Upendo Katika Ukristo Na Uislamu
40. Tiba Ya Maradhi Ya Kimaadili
41. Maana Ya Laana Na Kutukana Katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka Juu Ya Khofu
43. Kukusanya Swala Mbili
44. Bismillah Ni Sehemu Ya Qur'ani Na Husomwa Kwa Jahara
45. Kuwaongoza Vijana Wa Kizazi Kipya
46. Kusujudu Juu Ya Udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (S)
48. Tarawehe
49. Malumbano Baina Ya Sunni Na Shia
50. Kupunguza Swala Safarini
51. Kufungua Safarini
52. Umaasumu Wa Manabii
53. Qur'an Inatoa Changamoto
54. As-Salaatu Khayrun Mina -'N Nawm
55. Uadilifu Wa Masahaba
56. Dua E Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu Wa Binadamu
58. Umaasumu Wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu Wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu Wa Mitume - Umaasumu Wa Mtume Muhammad (S)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu Ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu Ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu Ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu Ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu Ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu Ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu Ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu Ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala Ni Nguzo Ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora Wa Imam 'Ali Juu Ya Maswahaba Na Ushia Ndio Njia Iliyonyooka
75. Hukumu Za Kifikihi Zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-U-Llaah
77. Muhammad (S) Mtume Wa Allah
78. Amani Na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani Na Mtume Muhammad (S)

81. Mitala Na Ndoa Za Mtume Muhammad (S)
82. Urejeo (Al-Raja'a )
83. Mazingira
84. Utokezo (Al - Badau)
85. Hukumu Ya Kujenga Juu Ya Makaburi
86. Swala Ya Maiti Na Kumlilia Maiti
87. Uislamu Na Uwingi Wa Dini
88. Mtoto Mwema
89. Adabu Za Sokoni
90. Johari Za Hekima Kwa Vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu Ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu Ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu Ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi Katika Usunni Na Ushia
96. Hukumu Za Mgonjwa
97. Sadaka Yenye Kuendelea
98. Msahafu Wa Imam Ali
99. Ngano Ya Kwamba Qur'ani Imebadilishwa
100. Idil Ghadiri
101. Kusoma Sura Zenye Sijda Ya Wajibu
102. Hukumu Zinazomuhusu Mkuu Wa Kazi Na Mfanyakazi
103. Huduma ya Afya katika Uislamu
104. Sunan an-Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Shahiid Mfiadini
108. Kumsalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Mariamu, yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
114. Hadithi ya Thaqalain
115. Ndoa ya Mutaa
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Mkutano wa Maulamaa wa Baghdad
122. Safari ya kuifuata Nuru



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 89 9/9/2015 12:56:09 PM

123. Fatima al-Zahra
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Elimu ya Ghaibu ya Maimamu
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Kwanza)
131. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Pili)
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu
135. yafaayo kijamii
136. Tabaruku
137. Taqiyya
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Visa vya wachamungu
141. Falsafa ya Dini
142. Azadari-Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
144. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu
151. Mafunzo ya hukumu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 1
153. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 3
155. Abu Huraira
156. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
157. Mazingatio kutoka katika Qur’an - Sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka kaitka Qur’an - Sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
161. Qur’ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
162. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
164. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu

165. Uislamu Safi
166. Majlisi za Imam Husein Majumbani
167. Je, Kufunga Mikono
168. Uislam wa Shia
169. Amali za Makka
170. Amali za Madina
171. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
172. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
173. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
174. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
175. Umoja wa Kiislamu na Furaha
176. Mas'ala ya Kifiqhi
177. Jifunze kusoma Qur'ani
178. As-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
179. Hayya 'Alaa Khayri'l-'Amal Katika Adhana
180. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
181. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhani)
182. Uadilifu katika Uislamu
183. Mahdi katika Sunna
184. Maswali ya Uchunguzi Kuhusu Uislam
185. Kazi na Bidii ni njia ya maendeleo
186. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
187. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
188. Vijana na Matarajio ya Baadaye
189. Usalafi – Historia yake, maana yake na lengo lake
190. Ushia – Hoja na Majibu
191. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
192. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
193. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
194. Takwa
195. Upotoshaji dhahiri katika Turathi (Hazina) ya Kiislamu
196. Amirul Muuminina ('as) na Makhalifa
197. Uongozi na Utawala katika Mwenendo wa Imam 'Ali ('a)
198. Kuvunja hoja iliyotumika kutetea Uimamu wa AbuBakr
199. Adabu za vikao na mazungumzo
200. Hija ya Kuaga
201. Uwazi baina ya Maslahi na Vikwazo
202. Fadhila za watukufu watano katika Sahih Sita
203. Mdahalo baina ya Mwanachuoni wa Kisunni na Mwanachuoni wa Kishia (*Al-Muraja'aat*)
204. Utawala na Uendeshaji katika Sera ya Imam Ali (as)
205. Mjadala wa Kiitikadi



09_15_KANUNI ZA SHARIA YA KIISLAM_9_September_2015.indd 91 9/9/2015 12:56:09 PM

206. Mtazamo kuhusu msuguano wa Kimadhehebu
207. Nchi na Uraia – Haki na wajibu kwa Taifa
208. Mtazamo wa Ibn Taymiyyah juu ya Imam Ali (as)
209. Uongozi wa Kidini – Maelekezo na Utekelezaji wa Kijamii
210. Maadili ya Ashura
211. Mshumaa – Shahidi na Kifo cha Kishahidi
212. Mizani ya Hekima – Hadithi za Ahlul Bait (as) – Sehemu ya Kwanza
213. Imam Ali na Mambo ya Umma
214. Imam Ali na Mfumo wa Usawa
215. Mwanamke na Sharia
216. Mfumo wa Wilaya
217. Vipi Tutaishinda Hofu?
218. Kumswalia Mtume ni Ufunguo wa Utatuzi wa Matatizo
219. Mahali na Mali za Umma
220. Nahjul-Balagha – Majmua ya Khutba, Amri, Barua, Risala, Mawaidha na Semi za
    Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib (a.s.)
221. Mukhtar – Shujaa aliyelipiza kisasi dhidi ya wauaji wa Imam Husein (as) hapo Karbala
222. Uimamu na Tamko la Kutawazwa
223. Imam Husain ni Mfumo wa Marekebisho na Mageuzi
224. Saada Kamili – Kitabu cha Kiada cha Maadili
225. Maeneo ya Umma na Mali Zake
226. Imam Hasan na Mfumo wa Kujenga Jamii
227. Adhana ni Ndoto au ni Wahyi?

## KOPI NNE ZIFUATAZO ZIMETAFSIRIWA KWA LUGHA KINYARWANDA

1. Amateka Na Aba'Khalifa
2. Nyuma yaho naje kuyoboka
3. Amavu n'amavuko by'ubushiya
4. Shiya na Hadithi

## ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION KWA LUGHA YA KIFARANSA

1. Livre Islamique